Pambazuko

Toleo Namba 086 | Jumatatu, Agosti 26 - Septemba 1, 2024

Fuatilia mfululizo wa makala za Afcon kila Jumatatu ukurasa wa 33 | Gazeti Maalum la Afcon 2027

Kishindo cha Ngorongoro

Bado 'Wamasai' hawajamalizana na serikali





Ni kizungumkuti, tulinde taswira ya nchi yetu isiharibike," alisema Dkt. Shoo

Habari Uk. 6 & 7

Dkt. Slaa:Tume Huru ya Uchaguzi kiini macho

Habari Uk. 14



Mbunge Kibiti kumpiga kofi Mwenyekiti CCM lisifunikwe

VYOMBO vikubwa vya habari Tanzania "havikuwa na muda" wa kuandika jambo hili, lakini ni vyema likawekwa rekodi....

Soma Uk. 11



Jeshi la Polisi kitanzini

HALI inayopitia Jeshi la Polisi Tanzania hivi sasa, inaweza kuelezwa kuwa chombo hicho cha kulinda usalama hakiko kwenye mwelekeo bora....

Habari Uk. 4

Upekee mfumo wa uchaguzi Marekani Uk. 16

Tahariri/Katuni

Maswali bado mengi Ngorongoro, yajibiwe

SAKATA la eneo la Ngorongoro; baina ya serikali na wakazi asilia wa eneo hilo, bado "linachemka."

Kwamba hadi sasa, bado halijapoa licha ya serikali kueleza kwamba baadhi ya mambo yaliyokuwa yakikoleza uhasama – kati ya wakazi na viongozi wao, sasa yamepatiwa ufumbuzi.

Baadhi ya mambo hayo ni kurejeshwa kwa huduma muhimu kwa binadamu; ikiwamo elimu, afya, na hata haki ya demokrasia iliyoonekana kupokwa kwa tamko la serikali hiyohiyo.

Akitangaza kurejeshwa kwa huduma hizo, Rais Samia Suluhu Hassan alisema wiki iliyopita kwamba serikali yake imeamua kurejesha huduma hizo ili maisha ya wakazi wa eneo hilo, yaendelee.

Kabla ya kauli ya Rais Samia, kulisambazwa taarifa rasmi ya serikali kwamba sehemu za eneo la Ngorongoro, Arusha, hakutakuwa na huduma za kijamii - zitaondoshwa, kwa kuwa tayari kuna msimamo wa serikali wa kuhamisha wakazi hao kwenda eneo jingine la Msomera, Handeni, Tanga.

Kutokana na msimamo huo wa sasa wa serikali, dhidi ya ule uliotolewa na serikali hiyohiyo, kunazua maswali mengi ambayo ni muda muafaka kujibiwa. Anayepaswa kuyajibu ni serikali yenyewe.


Pambazuko linapenda kuona serikali inapojibu maswali hayo, ieleze kwa umma wa Watanzania na dunia, kwa kujibu maswali yafuatayo.

Miongoni mwa maswali hayo ni nani hasa alizuia huduma kwa wananchi wa Ngorongoro? Alifanya hivyo kwa lengo gani? Alikuwa anamwakilisha nani wakati anachukua hatua hiyo kwa wenyeji wa Ngorongoro?

Je, nia hasa ilikuwa (au) ni kuondoa wakazi wote wa Tarafa ya Ngorongoro au kubakiza baadhi? Hawa waliopaza sauti na hata kuchukua njia ya maandamano ili kusikilizwa, kwanini hawakupewa nafasi tangu mwanzo kabla ya kufika huko?

Je, hawa walioshinikiza watu kuhama, wakiweka kauli laini kwamba – "ni kwa hiari," bado wako ofisi za umma, baada ya kauli ya Rais Samia na msimamo mpya wa serikali?

Hakika Pambazuko na umma wangependa kupata majibu haya ili isitokee tena kukarejewa kwa hatua za kulazimisha watu kuhama na serikali kuwa na kauli mbilimbili, kwa jambo moja.



Amiri Jeshi Mkuu...



Rais na Amiri Jeshi Mkuu, Samia Suluhu Hassan, akiwa kwenye picha ya pamoja na askari wa Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ) wakati wa kufunga zoezi la medani lililo-husisha vikundi mbalimbali vya askari wa jeshi hilo katika eneo la Pongwe Msungura, Msata mkoani Pwani mwishoni mwa wiki. (PICHA NA IKULU).

Jisajili kupata Pambazuko bure

- Ndugu msomaji wetu, jisajili kwa namba hii ya simu ya **WhatsApp: +255 744 768263** kwa kutuma neno **"HABARI"** kwa namba yako ya WhatsApp ili kupata Pambazuko kwenye WhatsApp yako.

- Pia unaweza kujisajili kwa kutumia **Email hii: info@pambazuko.or.tz** ili gazeti la Pambazuko likufikie kupitia email yako, andika neno **"HABARI"** na kutuma kwetu nawe utakuwa umejisajili.

Unaweza kusoma gazeti hili kupitia tovuti ya **www.rifaly.com**

TIMU YA PAMBAZUKO

Mhariri Mkuu	:	Simon **MKINA**	(simon@pambazuko.or.tz)
Mhariri Mtendaji	:	Peter **NYANJE**	0784 211 716
Mhariri wa Habari	:	Maregesi **PAUL**	0689 732 325
Mwandishi Mkuu	:	Elizabeth **HOMBO**	0712 792 216
Mkuu wa DTP	:	Yassin **LUPATU**	0782 009 971
Mkuu wa Utawala	:	Tryruckia **MFINANGA**	0744 768 263

Tunapatikana Pambazuko Initiative Office, Mtaa wa Mpakani A – nyuma ya Jengo la Sayansi. Kitalu Namba 435; Plot 44. Mawasiliano ya ofisi: Simu +255 744 768263 na Email: info@pambazuko.or.tz

Habari

Jeshi la Polisi sasa kitanzini



Msemaji wa Jeshi la Polisi nchini, David Misime

Na Na Mwandishi WETU

HALI inayopitia Jeshi la Polisi Tanzania hivi sasa, inaweza kuelezwa kuwa chombo hicho cha kulinda usalama hakiko kwenye mwelekeo bora wenye nadharia ya umoja kiutendaji.

Ukiacha kulalamikiwa kutokana na matukio kadhaa ya uhalifu, hivi karibuni imeshuhudiwa maofisa wa jeshi hilo wakitoa kauli rasmi, lakini muda mfupi baadaye jeshi linatangaza kutohusika nazo.

Hiyo inaleta picha kuwa jeshi hilo "halipo pamoja" kiundaji, kwani haiyumkini maofisa wake watoe taarifa zinazokinzana.

Hayo yanatokea wakati Jeshi la Polisi likiwa katikati ya malalamiko kutoka kwa watu na taasisi mbalimbali nchini kwa kile kinachoelezwa kuwa utendaji wake umeondoka katika mstari wa misingi ya sheria na katiba.

Yaliyojiri hivi karibuni baada ya maofisa wa jeshi hilo kushambulia viongozi wa upinzani umezidisha 'chuki' ya wananchi dhidi ya jeshi hilo.

Katikati ya madai ya watu kutaka jeshi hilo litoe taarifa kuhusiana na kupotea au kutekwa kwa watu nchini, juzi Msemaji wa Polisi, David Misime, alijitokeza hadharani ambapo alizungumzia mambo kadhaa bila kugusa hoja ambazo kwa siku za hivi karibuni ndio zimekuwa gumzo katika jamii zikilihusisha jeshi hilo.

Katika taarifa yake, Misime alizungumzia matukio ya utekaji na kutoa orodha ya watu watatu wanaodaiwa kutekwa kisha kuuawa, lakini hakuzungumzia wale waliotajwa katika orodha ya zaidi ya watu 80 wanaodaiwa kutekwa, iliyotolewa na Chama cha Wanasheria wa Tanganyika (TLS).

Baada ya kimya kirefu, Misime pia alitumia nafasi hiyo kuzungumzia suala la Ofisa wa Polisi, Fatma Kingondo, anayedaiwa kuwatuma vijana kumbaka binti aliyetajwa kuwa ni mkazi wa Yombo, Dar es Salaam, akieleza kuwa tayari faili lake limepelekwa kwa Mwendesha Mashtaka wa Serikali (DPP), kwa ajili ya taratibu nyingine za kisheria.

Misime anatoa taaifa hiyo baada ya kimya kirefu kilichowasukuma wanasheria kupeleka shauri mahakamani kutaka ofisa huyo akamatwe na kufunguliwa mashtaka.

Mmoja wa watu waliozungumza na Pambazuko ambaye amekuwa katika ngazi za juu za utendaji wa jeshi hilo na kwa sasa ni mstaafu (jina linahifadhiwa) alisema matukio haya ya hivi karibuni yanaonyesha kunahitajika mabadiliko ya haraka katika Jeshi la Polisi ili kurejesha imani ya wananchi kwa walinzi hawa wa usalama wa raia na mali zao.

Alisema waraka wa TLS, wa kutekwa na kuteswa kwa watu bila kuwafikisha mahakamani; kuteswa na kudhalilishwa kwa viongozi wa Chadema na sasa hili la msichana kufanyiwa unyama kingono, ni matukio ya wazi kabisa ya uvunjifu wa hali ya juu wa haki za binadamu.

"Ni bahati mbaya sana matukio yote haya yanawahusisha polisi moja kwa moja. Yaani polisi wanaotazamiwa kuhakikisha usalama wa raia na mali zao, ndio haohao wanaotuhumiwa kuhusika kuvunja haki za bindamu..."

"Rais asipochukua hatua madhubuti, nchi inaweza kutumbukia katika migogoro siyo ya lazima," alieleza.

Mwanasheria Eben Nderangusho aliliambia Pambazuko kuwa jeshi la Polisi lilipaswa kujifunza mambo kadhaa kutokana na yale yaliyohusisha kauli za viongozi wa juu wa Jeshi la Polisi, Camilius Wambura, ambaye ni mkuu wa jeshi hilo (IGP) na Ramadhani Kingai, Mkurugenzi wa Upelelezi wa Makosa ya Jinai

Inaendelea Uk. 12

Jicho la Tai

Aomba kazi kwa rais amalize hili la Ngorongoro

Na Igo Al

JANA, raia mmoja wa Tanzania aliita waandishi wa habari nyumbani kwake Kijitonyama, Dar es Salaam, kuwaomba wafikishe ujumbe wake kwa Rais Samia Suluhu Hassan.

Raia huyo aliyejitambulisha kuwa ni mstaafu, alieleza kwamba ana jambo mahsusi la kuisaidia Tanzania na watu wake ili waendelee kuishi kwa amani, umoja, na mshikamano; tunu alizoacha Mwalimu Julius Kambarage Nyerere – Rais wa Kwanza wa Tanganyika na baadaye Tanzania.



Mstaafu huyo aliyetaja jina lake kuwa ni Mzee Tai, alisema ameoteshwa kwamba viongozi wa Tanzania wasipochukua hatua za haraka sasa, nchi inaweza "kutumbukia shimoni" na kuingia kwenye machafuko.

Akasema, ili kuiokoa, ni lazima apatikane mtu ambaye anaweza kumaliza migogoro, chuki na manung'uniko ya wananchi dhidi ya serikali yao.

Mzee Tai akasema mwenye uwezo wa kuzuia machafuko yasitokee ni yeye. Kwamba ana uwezo, akili, ujuzi na uzoefu wa majukumu ya kijeshi "vinambeba" zaidi kwa kazi hiyo.

Mzee huyo wa makamo akadai kuwa ili kuonyesha kwamba anaweza kazi, apewe kazi moja tu; ya kukabili na kuzimaliza chokochoko za wakazi wa Tarafa ya Ngorongoro.

Kwamba kile kinachoitwa minyukano ama vurugu za wakazi wa Ngorongoro dhidi ya serikali yao, anaweza kukimaliza kwa dakika chache mno, baada ya kupokea barua ya ajira kutoka kwa Rais Samia.

Je, yeye atafanya nini hasa kumaliza minyukano ya wafugaji, jamii ya Wamasai na serikali yao huko Ngorongoro? Hili ndilo swali alilo-ulizwa na mmoja wa waandishi wa habari alio-waalika.

Awali Mzee Tai alikataa katakata kujibu swali hilo, akidai kwamba ni siri yake, kwani akiliweka hadharani, anaweza kutokea "mjanja" akamuwahi kwa Rais Samia na kupewa ajira.

Hata hivyo, baada ya kubanwa sana, kwa sauti ya chini, akatoa jibu; "nitawaacha wafugaji wa Ngorongoro, waendelee kuishi na wanyamapori. Simple!"

Tutumie tafsiri yako ushinde...



Huu ni mchoro wenye maana kubwa. Kila mmoja anaweza kuwa na tafsiri yake, hivyo gazeti la Pambazuko linatafuta tafsiri fupi, inayoelezeka na kufafanua vyema kuliko zote na itachapishwa na gazeti hili kwenye Ukurasa wa 30 toleo linalofuata. Mhusika atatumiwa zawadi – Tuma tafsiri yako kwa simu: 0744 768 263 .

Habari Kuu

Kishindo cha wakazi Ngorongoro



Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge na Uratibu), William Lukuvi akizungumza na wananchi wa Ngorongoro wiki iliyopita. (Na Mpigapicha Wetu)

Na Mwandishi WETU

KAULI ya Rais Samia Suluhu Hassan "kuzima" mgogoro wa wakazi wa eneo la Ngorongoro, bado haijamaliza tatizo la kimkakati lililotengenezwa na serikali.

Inaweza kuonekana kauli hiyo ya kiongozi wa nchi inaondoa vikwazo na kusimamisha kero walizokuwa wakipata wakazi wa Ngorongoro, baada ya kusimamishiwa huduma za kijamii na serikali, lakini kumbe bado kuna kilio kutoka kwa wakazi wa asili wa eneo hilo, wengi wakiwa ni wafugaji.

Wiki iliyopita, Rais Samia aliamuru kurejeshwa kwa huduma za kijamii katika Tarafa ya Ngorongoro, Mkoa wa Arusha, ambazo zilisitishwa na serikali kwa lengo la kushinikiza wakazi hao kuhamia Msomera, wilayani Handeni, Tanga.

Wakazi hao ambao serikali inawataka wahame kutoka katika eneo hilo kama sehemu ya kuhifadhi Bonde la Ngorongoro, wametoa angalizo kwa serikali wakisema iwapo ahadi zinazotolewa hazitatekelezwa kikamilifu, wao wataendelea na msimamo wa kuishinikiza serikali kuwatambua na kuwathamni.

Walisema kwa muda wa miaka mingi wao wamekuwa ni walinzi wa wanyama, mazingira na ikolojia ya eneo hilo, lakini sasa wanaauriwa kuondoka ili kuwepo kwa shughuli zingine ambazo zitakuwa chanzo cha kuharibu mambo hayo.

Aidha, pamoja na ahadi zilizotolewa na serikali kupitia Rais Samia, wakazi hao nao wamekuja na orodha ya mambo wanayotaka yafanyike ili kulifanya eneo hilo kuwa salama zaidi kwao na kwa wanyama.

Wakizungumza na Pambazuko siku moja baada ya mawaziri kadhaa kuzuru eneo hilo na kutangaza uamuzi wa serikali kurejesha huduma za jamii, wafugaji hao wamesema kuwa hawatakubali kunyanyaswa kwa sababu wanazifahamu haki zao.

Wameitaka serikali kuhakikisha kuwa badala ya kuwasumbua wao, iachane na baadhi ya miradi ya maendeleo katika eneo hilo kwani hiyo ndiyo tishio zaidi kwa mazingira na ikolojia ya bonde hilo kuliko wao.

Diwani wa Kata ya Alaitole, James Moringe, ameliambia Pambazuko kuwa miradi ya uwekezaji katika tarafa yao inapaswa kuangaliwa upya kwa kuwa baadhi ya wawekezaji wamejenga hoteli za kitalii bila kuwashirikisha wananchi wa maeneo husika.

"Kwanza kabisa namshukuru Rais Samia kwa kumaliza mvutano uliokuwapo kwa amani, huku akiagiza tuendelee kuishi katika makazi yetu kama kawaida na huduma zote za kijamii zirudishwe.

"Lakini ili kuepuka migogoro isiyokuwa na maana kati yetu na serikali, pamoja na wawekezaji, umefika muda sasa mahoteli yote yaliyojengwa katika mapito ya wanyamapori na kwenye mapito ya mifugo yetu, yaondolewe kwa sababu yalijengwa bila kufuata utaratibu,"amesema.

Amebainisha kuwa miradi kama hiyo imejengwa katika kata za Misigiyo na Ngoile ambako kuna hoteli zimejengwa katika mapito ya wanyamapori na katika maeneo wanayopitisha mifungo yao.

Kiongozi huyo amesema wamekuwa wakilalamikia jambo hilo kwa muda mrefu, lakini hakuna hatua zilizochukuliwa zaidi ya kuwahamisha wafugaji.

"Pamoja na uwepo wa mahoteli hayo, kuna mwongozo wetu wa kuanzia mwaka 2006 hadi 2016, ambao unazuia uwekezaji katika maeneo fu-

Inaendelea Uk. 7

Kishindo cha wakazi Ngorongoro

Inatoka Uk. 6

lani fulani, lakini makubaliano hayo yanavunjwa na watu bila sababu za msingi," ameongeza kusema.

Ametahadharisha; "kwa hiyo, kuanzia sasa, wawekezaji watakaotaka kuwekeza kwetu, wapate kibali cha wananchi wa maeneo husika kwa sababu bila kufanya hivyo, inaweza kuibuka migogoro isiyokuwa na maana."

Kwa mujibu wa diwani huyo, uwekezaji usiofuata utaratibu, unaweza kuharibu uhalisia wa eneo la Ngorongoro, jambo ambalo alisema wananchi hawataki litokee.

Akizungumzia kurejeshwa huduma za kijamii kama Rais Samia alivyoagiza, amesema wakazi wa Tarafa ya Ngorongoro wanasubiri kutekelezwa kwa ahadi hiyo kwa sababu wameteseka kwa muda mrefu.

"Tunaamini agizo la Rais Samia litatekelezwa haraka kwa kurejeshwa huduma za maji, afya, elimu na nyinginezo. Tunataka pia ile shule yetu ya wasichana (Ngorongoro Girls), iboreshwe kwa sababu mazingira yake siyo rafiki kwa wanafunzi wa kike kwa sasa," amesisitiza.

Katika hatua nyingine, alisema kuanzia leo, viongozi wote katika tarafa hiyo, wakiwamo madiwani na maofisa watendaji, wameitisha mikutano ya hadhara katika maeneo yao kuwaeleza wananchi umuhimu wa kusahau yaliyopita na kuhimiza masuala ya maendeleo ikiwa ni pamoja na kushiriki kwa wingi upigaji kura katika uchaguzi wa Serikali za Mitaa unaotarajia kufanyika Novemba 27, mwaka huu.

Hatua hiyo ya serikali kurejesha huduma katika tarafa hiyo imefuatia sintofahamu iliyoibuka baada ya majina ya wakazi wa eneo hilo katika daftari la kudumu la wapigakura kuhamishiwa



katika Kijiji cha Msomera, Wilaya ya Handeni, Mkoa wa Tanga.

Hatua hiyo ilifuatiwa na tangazo la serikali kupitia Waziri wa Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), Mohamed Mchengerwa, kutangaza kuvifuta vijiji na vitongoji vyote katika tarafa hiyo.

Kabla ya hapo serikali ilisitisha huduma zote za kijamii katika eneo hilo baada ya wakazi hao kugoma kuhamia Msomera kama ambavyo wamefanya wenzao wapatao 9,600.

Mapema wiki iliyopita, wakazi hao walifanya maandamano ya amani wakidai kurejeshwa kwa huduma za jamii katika tarafa yao na pia kurejeshwa kwa vituo vya kupigia kura.

Walisisitiza kuwa hawataki kuonana na kiongozi mwingine yeyote zaidi ya Rais Samia kwa sababu viongozi wengine wa ngazi za chini, wamekuwa wakiwapa ahadi ambazo hazitekelezwi.

Maelfu ya wakazi hao waliamua "kushinda" barabarani kwa takribani siku tano wakiishinikiza serikali kubadili msimamo wake wa kutaka kuwaondoa.

Inaendelea Uk. 8

rifaly
Habarika kidijitali! Soma gazeti la Pambazuko na magazeti mengine maarufu kwenye Rifaly!
Scan to download Rifaly
www.rifaly.com

Habari Kuu

Kishindo cha wakazi Ngorongoro

Inatoka Uk. 7

Kitendo cha wananchi hao kukusanyika, kilimfanya Rais Samia kuwatuma Ngorongoro mawaziri waandamizi katika Baraza lake la Mawaziri, William Lukuvi (Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Uratibu wa Bunge) na Waziri wa Katiba na Sheria, Profesa Palamagamba Kabudi, kwenda kuzungumza nao.

Mawaziri hao walikutana na wananchi hao Ijumaa na kutangaza kuwa Rais Samia ameagiza huduma zote zilizokuwa zimesitishwa katika tarafa hiyo zirejeshwe vikiwamo na vituo vya kupigia kura.

Kanisa Katoliki lanena

Shinikizo la kuitaka serikali kuwasikiliza wananchi hao lilitiwa nguvu na kauli iliyotolewa na Rais wa Baraza la Maaskofu Tanzania (TEC), Askofu Wolfgang Pisa, wakati wa Jubilei ya Fedha ya Askofu Anthon Langwen wa Mbulu.

Katika kauli yake, Askofu Pisa aliitaka serikali kuzungumza na wananchi hao badala ya kufuta maeneo ya makazi yao.

Kwa mujibu wa Askofu Pisa ambaye pia ni Askofu wa Jimbo Katoliki la Lindi, nchi inayoongozwa kwa mfumo wa utawala bora, haiwezi kuwanyima huduma za kijamii wananchi wake kama ilivyotokea Ngorongoro.

"Uhalali wa uongozi katika utawala bora, unatoka kwa wananchi wenyewe na kwa kuwa madaraka ya viongozi yanatoka kwa watu, viongozi hao wanawajibika kwa wananchi jinsi wanavyotumia madaraka yao.," alisema Askofu Pisa.

Akaongeza; "kwenye nchi iliyojengwa kwa utawala bora kwa yale yanayotokea Ngorongoro, tunaiomba serikali ikae meza moja na watu wa Ngorongoro, iwasikilize, isiwalazimishe kuhama, wala kuwakosesha huduma muhimu za jamii au kuzuia chakula kuwafikia."

Mtumishi huyo wa Mungu, alisema wananchi hao pia wapewe haki yao ya kupiga kura mahali walipo, huku viongozi wakihakikisha kuwa wanalinda sheria, haki na ukweli kwa sababu ni vigumu kuwaeleza Watanzania kuwa Wamasai wanahama kwa hiari yao, halafu kesho yake tunaona Wamasai wamejaa barabarani wakilia na kupaza sauti zao wakidai kuporwa haki zao.

Maoni ya Askofu Dkt. Shoo

Aliyekuwa Mkuu wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT), Askofu Dkt. Frederick Shoo, aliliambia Pambazuko kwa simu kuwa kinachoendelea Ngorongoro ni kizungumkuti na kwamba taswira ya nchi inapaswa kulindwa.

"Ni kizungumkuti, tulinde taswira ya nchi yetu isiharibike," alisema Dkt. Shoo (pichani), ambaye pia ni Mkuu wa Dayosisi ya Kaskazini.

Mashirika 27 yaonya

Mashirika 27 yanayofanya kazi katika eneo hilo nayo yalitoa tamko yakilaani kitendo cha serikali kuwanyima wananchi hao haki ya kupiga kura.

Mashirika hayo yalisema katika taarifa yao kwa vyombo vya habari kuwa kufanya hivyo ni sawa na kuwalazimisha wananchi hao kuhama eneo hilo.

Mashirika yaliyotoa tamko hilo ni pamoja na Mtandao wa Watetezi wa Haki za Binadamu Tanzania (THRDC), Jukwaa la Katiba Tanzania (Jukata), Haki Ardhi, Chama cha Wafugaji Tanzania, Shirika la Utafiti wa Kijamii na Huduma za Maendeleo (CORDs) na Baraza la Wafugaji Wanawake (PWC).

Freeeman Mbowe

Kwa upande wake, Mwenyekiti wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema), Freeman Mbowe, alikipongeza Chama cha Wanasheria wa Tanganyika (TLS), wanasheria mbalimbali, viongozi wa dini pamoja na watu mbalimbali waliojitokeza kuzungumzia na kulaani ukiukwaji wa haki uliokuwa ukiendelea Ngorongoro.



Mbowe alisema eneo lilolofutwa na serikali ni makazi ya asili ya jamii ya Wamasai ambao wanastahili kuheshimiwa kwa kuwa ni Watanzania.

Mezani kwa Chahali

Na Evarist Chahali
evarist@chahali.com



Msimamo wa 'Wamasai' uwe mwangwi kwa wapinzani



Wakazi wa Ngorongoro wakiwasikiliza viongozi wa serikali waliojitokeza kutatua mgogoro wao hivi karibuni. (Picha na Mtandao)

HABARI iliyotawala sana wiki iliyopita – katika maeneo mengi, siyo Tanzania pekee, ni kuendelea kuwepo kwa mgogoro wa eneo la Ngorongoro.

Mgogoro huo ambao umedumu miaka mingi, huku njia nyingi zikutumika kuutatua, lakini haukuwahi kufikia hatua iliyofikiwa wiki iliyopita.

Mgogoro huo umesababisha kuibuka kwa mijadala mikali kuhusu haki za binadamu nchini Tanzania, hususan kuhusu mpango wa serikali kuwahamisha wakazi wa wneo hilo, wengi wakiwa ni "Wamasai" kutoka kwenye ardhi yao ya asili kwa ajili ya kuendeleza shughuli za utalii na uwekezaji wa kigeni.

Kumeibuka maswali mengi kuhusu haki za jamii za asili na ni nani anayepaswa kuamua kuhusu matumizi ya ardhi ya eneo hilo.

Wamasai, ambao wameishi Ngorongoro kwa karne nyingi, wanakabiliwa na tishio la kupoteza ardhi yao, ambayo ni sehemu muhimu ya utamaduni na maisha yao.

Lengo la makala haya ni kueleza kitu ambacho Waingereza wanaita "unintended consequences" yaani matokeo ambayo hayakukusudiwa.

Jambo moja lililojitokeza kutokana na mgogoro huo, ni jinsi jamii ya Kimasai huko Ngorongoro ilivyofanya kile ambacho hata vyama vya upinzani vimeshindwa kufanya.

Kwamba jamii ya wakazi wa Ngorongoro wakaamua kuungana na kusimama kidete dhidi ya ukandamizwaji wa haki zao.

Na jitihada zao zimezaa matunda baada ya serikali kuchukua hatua kadhaa kutatua mgogoro huo.

Kingine, mgogoro huo unaweza kuwa umewapatia wapinzani hoja muhimu katika kampeni zao. Kwa kuonyesha jinsi Chama Cha Mapinduzi (CCM) ilivyoshindwa kulinda haki za binadamu na kuwalinda Wamasai.

Sasa vyama vya upinzani vinaweza kuleta ujumbe mzito kwa wapigakura kwamba chama hicho tawala kimepoteza uhalali wa kuendelea kuongoza nchi.

Serikali inapotumia nguvu kuwahamisha Wamasai, inaonyesha udhaifu wa kimaadili na ukosefu wa kujali haki za raia wake.

Hili ni jambo ambalo linaweza kutumiwa na upinzani kuonyesha kuwa CCM siyo chama kinachowajali wananchi wake, bali kinawapuuza kwa maslahi ya wachache.

Uhamishaji wa Wamasai umesababisha maumivu makubwa kwa jamii hiyo, na hili linaweza kutafsiriwa kama mfano wa jinsi CCM ilivyo mbali na watu wa kawaida.

Katika hotuba na kampeni zao, vyama vya upinzani vinaweza kuishtaki CCM mbele ya wananchi kwa kigezo cha yaliyojiri huko Ngorongoro.

Ikumbukwe pia kuwa wakati mgogoro wa Ngorongoro ulipofika hatua ya juu, kulikuwa na matukio mengine ambayo yanaweza kuhusishwa na upungufu ndani ya chama hicho tawala, CCM.

Matukio hayo ni kama yale ya kupotea kwa watu mbalimbali sambamba na wimbi la ubakaji dhidi ya watoto.

Pamoja na matukio mengine ya ukiukwaji wa haki za binadamu, vyama vya upinzani vinaweza kujenga picha ya kwamba Serikali - inayosimamiwa na CCM, ilivyoshindwa kulinda haki za wananchi.

https://instagram.com/evarist_chahali

Tafakuri ya Bagonza



Sasa ni wakati kuhitaji nguvu ili kuharibu

Na Dkt. Benson BAGONZA

JOHN Malecela, ambaye aliwahi kuwa Waziri Mkuu wa Tanzania, yuko kwenye kumbukumbu akisema; “urais siyo kubeba karai la zege.”

Kiongozi huyo alimaanisha uongozi hauhitaji kutumia misuli na mitulinga.

Hata hivyo, alisahau ama alipitiwa kwamba mara nyingi tunahitaji kutumia nguvu ili kuharibu. Ili kujenga, kupatanisha, kutenda haki, kuridhiana na kutunza amani, tunahitaji hekima tu.

Suala la Ngorongoro linahitaji hekima, siyo nguvu. Linahitaji kushindwa, siyo kushinda. Linajitaji kujishinda, siyo kuwashinda wengine. Linahitaji kusikiliza watu (siyo washauri) kuliko kusema.

Nilichelewa kuilaumu serikali na nitachelewa kuipongeza. Kwa nini?

Mosi, Rais Samia Suluhu Hassan alikuwa anahubiri 4R wakati watendaji wa serikali wakitumia misuli, hila, mizengwe, wasanii, na wana habari ndumila kuwili.

Najua nakosea kumtenga rais na serikali yake, lakini nafanya makusudi ili kuwaonya watendaji wasiojielewa. Ipo siku watageuka nyuma wakute rais hayupo.

Pili, suala la Ngorongoro linatishia kuchafua usafi wa mihimili na vyombo vingine nyeti. Tusitishe matumizi ya nguvu na kuondoa pazia za usiri ili kudumisha amani.

Ieleweke kuwa watu wema hufurahia nuru. Waovu hupenda giza.

Tatu, wateule wa rais waliotumwa kupeleka habari njema Ngorongoro amekosekana mmoja wa Tamisemi.

Kura ndilo daraja kati ya wananchi na watawala wetu. Bila kura, serikali inakosa uhalali wa kuwaambia chochote wananchi. Daraja hilo (Tamisemi) limedhohofika.

Tufikiri upya katika muktadha wa maridhiano. Imani ikikosekana, hakuna njia ya kuonekana haki inatendeka.

Nne, kama Ngorogoro pametulia, rais ageuze shingo na kutazama mahali pengine panapofuka moshi.

Tumtibu njiwa akiwa bado na uwezo wa kuruka. Kuna ‘mioshi’ maeneo mengi na nguvu haifai tena. Hekima tu ndiyo inahitajika kurejesha imani ya wananchi kwa watendaji.

Mwandishi wa safu hii ni Askofu wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT), Jimbo la Karagwe. Ni mchangiaji maalum wa safu na makala ndani ya Pambazuko.

Mwandishi wa safu hii ni Askofu wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT), Jimbo la Karagwe. Ni mchangiaji maalum wa safu na makala ndani ya Pambazuko.



Hoja Yangu

Na Rashid MTAGALUKA

Mbunge Kibiti kumpiga kofi Mwenyekiti CCM lisifunikwe

VYOMBO vikubwa vya habari Tanzania "havikuwa na muda" wa kuandika jambo hili, lakini ni vyema likawekwa kwenye rekodi sahihi ili kudhibiti matukio ya namna hii.

Hakika umma umepokea kwa masikitiko makubwa taarifa za Mbunge wa Jimbo la Kibiti, Pwani, Twaha Mpembenuwe kumlamba kofi Mwenyekiti wa Umoja wa Vijana wa Chama Cha Mapinduzi (UV-CCM), Wilaya ya Kibiti, Amina Mkomboya.

Baadhi ya viongozi wa UV-CCM Kata ya Bungu wanaoonekana wakizungumza kwa masikitiko kwenye mitandao ya kijamii, baada ya mbunge huyo kutekeleza jinai hiyo huko Kibiti wakiwa kwenye kikao cha kamati ya siasa cha wilaya hiyo hivi karibuni.

Kabla ya kuandika, nilizungumza - kwa njia ya simu, na mbunge huyo ambaye alikiri kutokea kwa shambulio hilo, lakini alisema ni suala la kichama na kwa hiyo limemalizwa ki-chama, na iwapo mwandishi anahitaji maelezo zaidi awafuate viongozi wa chama.

Inashangaza kwamba mbunge anasema kumpiga 'vibao' mwenyekiti wa jumuia ya chama kilichomdhamini kugombea ubunge ni la kichama, lakini sheria inaliona ni suala la kijinai lisilopaswa kumalizwa kimyakimya, vinginevyo CCM inafungua mlango wa wabunge kwenye majimbo kuwaonea viongozi wa jumuia za chama hicho.

Kibaya zaidi vijana na wanachama wengine wa CCM wilayani Kibiti wanamshangaa mbunge huyo "kufanya ujanja" na kushawishi 'wakubwa' kumsimamsisha uongozi aliyezabwa vibao!

Inadaiwa kuwa mbunge alipandwa hasira baada ya kutofautiana kauli na Amina, hivyo kujichukulia sheria mkononi.

Kimsingi, sheria za Tanzania zinazuia mtu yeyote kujeruhi mwenzake kwa sababu yoyote ile, lakini sasa mtunga sheria, ndiye anahusika kuzivunja.

Hivi Mpembenuwe anajua kwamba, UV-CCM ni ndiyo injini ya chama hicho tawala katika kukipigania ushindi wake? Iweje sasa anavuruga wapiganaji wake?

Mpembenuwe anafahamu kwamba, vijana alioanzisha nao 'bifu' ni watoto wa kina mama wa Kibiti wanaounda Umoja wa Wanawake (UWT)? Na je, anaelewa kwamba vijana anaopambana nao Kibiti ndiyo jeuri ya CCM kwa Mkoa wa Pwani?

Vijana wamejaribu kupaza sauti zao kwa viongozi wa CCM ngazi ya mkoa hadi taifa ili kusaidia hali ya chama wilayani, lakini taarifa zinaeleza kuwa "hawajasikilizwa" na kuwa chanzo cha kutokea kwa mivurugano na kudhoofisha umoja uliopo miongoni mwa wanachama wa chama hicho tawala.

Inawezekana wakubwa wameamua kulikalia kimya suala hili kulinda chama kisiparaganyike huko Kibiti na Pwani, lakini hoja yangu ni kwamba, CCM ina mengi ya kuyafunika ila siyo hili, hasa kipindi hiki cha kuelekea kwenye uchaguzi wa mitaa na uchaguzi mkuu mwakani, 2025.

Rashid Mtagaluka ni mwandishi wa habari na anapatikana kwa simu nambari 0784 438 546 na email; mtagaluka@gmail.com



Mbunge wa Jimbo la Kibiti, Twaha Mpembenuwe

Habari

Jeshi la Polisi...

Inatoka Uk. 4

(DCI) katika kesi ya ugaidi dhidi ya Mbowe.

Hata hivyo, pamoja na kuibuka kwa malaamiko kuhusu kesi hiyo, iliwashangaza watu wengi kuwa vigogo hao walipopandishwa vyeo wakati waliyoyafanya katika kesi hiyo yaliacha fedheha kubwa kwa jeshi hilo.

Makanusho

Moja kati ya matukio yaliyoshusha hadhi ya jeshi hilo hivi karibuni ni hatua ya Polisi Wilaya ya Mbagala, kupiga marufuku mikutano ya vyama vya siasa kupitia majibu ya barua iliyoandikwa na chama cha ACT-Wazalendo iliyoomba kufanya mkutano katika eneo hilo.

Barua hiyo ilijibiwa na Kaimu Mkuu wa Polisi (W) Mbagala, Robe John.

Majibu yake yalisomeka hivi; “Pamoja na barua hii napenda kukujulisha kuwa mikutano yote ya hadhara na ya ndani imezuiliwa hadi hapo yatakapotolewa maelekezo mengine.”

Siku moja baadaye barua hiyo ilikanushwa na Msemaji wa Polisi, Misime, ambaye alitoa taarifa kwa umma akieleza kuwa jeshi hilo halijapiga marufuku kufanyika mikutano ya nje na ya hadhara ya vyama vya siasa.

“Kilichopigwa marufuku ni mkusanyiko uliokuwa umeitishwa na viongozi wa Chadema huko jijini Mbeya kwa kivuli cha kuadhimisha Siku ya Vijana Duniani,” alieleza Misime.

Katika tukio jingine, Agosti 19 mwaka huu Jeshi la Polisi lililazimika kukanusha taarifa iliyotolewa na aliyekuwa kiongozi wa jeshi hilo Mkoa wa Dodoma, Kamishna Msaidizi Mwandamizi (SACP) Theopista Mallya, ambaye alikaririwa akisema kuwa “binti anayedaiwa kubakwa na kulawitiwa alikuwa kama anajiuza.” Kauli hiyo ya Mallya aliyoitoa katika mazungumzo yake na mwandishi wa habari ilimgharimu baada ya msemaji wa jeshi hilo kutoa taarifa kuwa kuwa kauli hiyo siyo msimamo wa Jeshi la Polisi.

Kwa kuonyesha kuwa huo kweli haukuwa msimamo wa jeshi hilo, IGP alitangaza kumwondoa Mallya kwenye wadhifa wake na kumrudisha makao makuu ya jeshi hilo.

Aidha, siku iliyofuata, vijana wanatuhumiwa kufanya hivyo wakafishwa mahakamani jijini Dodoma.

Wanasiasa nao

Ukiacha hayo, pia wapo baadhi ya watu maarufu nchini ambao wamelituhumu jeshi hilo kwamba limekosa weledi.

Mmoja wao ni Makamu wa Kwanza wa Rais Zanzibar, Othman Masoud Othman, ambaye wiki iliyopita alilitaka jeshi hilo kuacha kufanya kazi kisiasa.

Othman, ambaye pia ni Mwenyekiti wa Chama cha ACT –Wazalendo Taifa, alilitaka Jeshi la Polisi kuacha vitisho dhidi ya viongozi wa chama hicho na kufanya kazi zao kwa uadilifu, bila kuegemea upande mmoja wa kisiasa.Othman alisema ni wazi kwamba vitisho kutoka kwa Kamshina wa Polisi Zanzibar, Hamad Khamis, dhidi ya viongozi wa chama hicho, vina msukumo wa kisiasa kutoka kwa viongozi walioelemewa na hoja za chama hicho.

Alishangazwa ni kwa namna gani jeshi ambalo linapaswa kufanya kazi kwa weledi bila upendeleo wa kisiasa, limeanza kuwanyanyasa baadhi ya wananchi kwa kuzingatia tofauti za kisiasa.

Othman alisema wakati akizungumza na waandishi wa habari katika ofisi za chama hicho, Zanzibar kuwa kinachofanywa na Jeshi la Polisi hivi sasa visiwani humo, kinadhihirisha kuwa limepoteza uaminifu. Alisema inashangaza kuwa kuna matukio ya uhalifu mkubwa ambao yametolewa maelezo na ushahidi na chama hicho, lakini Jeshi la Polisi halijachukua hatua zozote badala yake linatoa vitisho kwa viongozi wa chama chake.

Alisema iwapo jeshi hilo lingekuwa na dhamira ya kweli ya kudhibiti uvunjifu wa amani na kwa vile jinai haina ukomo, polisi walipaswa kuchuka hatua ikiwemo kuchunguza kuuawa kwa watu 21 katika maeneo mbali mbali ya visiwa vya Unguja na Pemba katika miezi ya Oktoba na Novemba mwaka 2020 kwenye uchaguzi wa mwaka huo.

Alieleza kuwa licha ya kuyafahamu mauaji hayo, polisi wameshindwa hata kufungua jalada dhidi ya matendo hayo angalau kwa uchunguzi.

Kwa upande wake, Mwenyekiti wa Chadema, Freeman Mbowe, yeye alikwenda mbali zaidi katika mkutano wake na waandishi wa habari kwa kuwataja baadhi ya maofisa wa Jeshi la Polisi akiwatuhumu kuongoza genge la watekaji.

Mbowe alituhumu kuwa lilipoanzishwa, kundi hilo lililenga kupambana na uhalifu, lakini sasa limegeuzwa kuwa la utekaji wa watu ambao wana msimamo tofauti na watawala.

Kona ya Dkt. Bisimba



Hivi hatuwezi kufikiri demokrasia mbadala?

Na Dkt. Hellen Kijo
BISIMBA



Vitendo vya utekaji

KUNA hali isiyo ya kufurahisha katika kipindi hiki kuelekea kujiandaa kufanya Uchaguzi wa Serikali za Mitaa mwishoni mwa mwaka huu na Uchaguzi Mkuu baadaye mwakani.

Yapo mambo mengi ya kusikitisha yanatokea kwa sasa ikiwamo utekaji na kupotea kwa watu.

Jeshi la Polisi linalaumiwa na kutuhumiwa kuhusika na utekaji huo, kwa kuwa linadaiwa kukamata watu kimya kimya.

Wapo watu kadhaa ambao walipotea katika mazingira ya kutatanisha, lakini baadaye jehi hilo likatangaza kuwa linawashikilia.

Hivi sasa kuna gumzo kuhusu kijana Deo Soka, ambaye hajulikani alipo. Taarifa zilizopo zinasema kabla ya kupotea alipokea wito kutoka jeshi hilo akitakwia akachukue pikipiki yake.

Hali hii inaibuka wakati wengi tulishaamini kuwa tumepita kwenye enzi hizo.

Ukijumlisha na suala lililomkumba binti aliyetendewa uovu na watu waliosemekana walitumwa na 'afande' na majibu yaliyotolewa na kiongozi wa jeshi hilo, yanaashiria kuna walakini mkubwa sana katika masuala ya kiutawala na hata kiuongozi.

Kuhamishwa watu kwa lazima huko Ngorongoro huku tukitangaziwa kuwa kuhama ni hiari, ni kiini macho kingine cha kiutawala na kiuongozi.

Najiuliza hivi ni vipi nchi yenye utawala wa kidemokrasia inakuwa na mambo haya? Wanachi wana wawakilishi ambao ni wabunge na madiwani na hata wajumbe wa serikali za mitaa.

Je, nafasi ya hawa wawakilishi pale ambapo serikali ndiyo inanyooshewa kidole ni ipi?

Katika hali ambayo serikali inaonekana kushindwa kutimiza wajibu wake wa kulinda raia na mali zao kiasi hata cha kuwa na mikataba inaonyesha kutuhujumu kama taifa, tulitarajia wawakilishi wetu ndiyo wainuke, kuikemea na kuiongoza serikali. Hili halijafanyika.

Inashangaza kuwa wawakilishi hawa wanachaguliwa na wananchi kupitia vyama vyao vya siasa, lakini wanapofika katika mabaraza wanawasahau kabisa wananchi na kujali maslahi yao binafsi.

Bahati mbaya zaidi chama kinachopata ushindi ndicho kinachounda serikali ambayo inajitambulisha kama serikali ya chama hicho.

Hapo serikali inajiwekea kinga kupitia chama chake. Katika hali kama hii wabunge kutoka chama hicho hawawezi tena kuihoji serikali inaposhindwa kutekeleza majukumu yake.

Katika utafiti kidogo nilioufanya nimegundua kuanza kwa mfumo wa demokrasia hakukuwa na vyama vya siasa, bali watu walikuwa wakitengeneza sheria kwa njia tofauti za kura zao moja kwa moja.

Nimeangalia nchi chache ambazo hazina vyama vya siasa zikiwemo zenye tawala za kifalme, lakini zipo ambazo ni demokrasia bila vyama kama - Tuvalu na Palau - nchi ndogo sana.

Kwa kuangalia nchi hizi nikawaza kuwa pengine nasi tunaweza kuachana na vyama vya siasa ambavyo vimethibitisha kuwa kazi yao kubwa ni kutafuta kutawala wakati wananchi tunataka kuongozwa.

Viongozi wengi tunaoapata chini ya mfumo tulionao, hawatekelezi yale waliyotuahidi.

Wananchi wanaishi kwa hofu ya kutekwa, kuondolewa unakoishi, kufanyiwa ukatili, kutofaidi rasilimali huku viongozi wakipigania maslahi binafsi.

Naona vyama vimetuangusha ,tushike usukani wenyewe kwa kutafuta demokrasia mbadala.

Mwandishi wa safu hii ya kila wiki, ni mwanaharakati wa demokrasia, haki za binadamu na mwanazuoni wa falsafa ya sheria. Anapatikana kwa namba 0713 337240.

Ana kwa Ana

Slaa: Tume Huru ya Uchaguzi kiini macho

KATI ya wanasiasa waliotikisa katika siasa za upinzani Tanzania ni Dkt. Wilbrod Slaa ambaye aliwahi kuwa katibu mkuu wa chama kikubwa cha upinzani nchini, Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema).

Kabla ya hapo aliwahi kuwa Padre wa Kanisa Katoliki, lakini taaluma yake ya sheria ilimfanya aaminiwe na aliyekuwa Rais wa Tanzania, John Magufuli aliyemteua kuwa balozi.

Hivi karibuni waandishi wa Pambazuko walipata wasaa wa kukaa pamoja na kumuhoji kiongozi huyu na yafuatayo ni maswali na majibu; endelea...

Pambazuko: Hivi karibuni ulitangaza kuachana na siasa za vyama na kuwa mshauri huru wa masuala ya kisiasa. Historia yako kisiasa, ulianzia CCM, ukatoka ukaingia Chadema, ukapata nafasi za juu, ukarudi CCM. Unaonekana kama mtu asiye na msimamo mwenye kutafuta maslahi binafsi. Unadhani watu watakuamini?

Dkt. Slaa: Tatizo ni kuwa Watanzania wengi, hata ninyi waandishi wa habari, hamjui siasa.

Labda nikupe historia yangu kwenye siasa na utumishi kwa ufupi. Nimekuwa kwenye siasa kuanzia 1973 wakati wa TANU nikiwa katiba wa tawi la TANU, maana CCM wakati huo ilikuwa haijaanzishwa.

Niliingia humo kwa sababu ndicho chama pekee kulichokuwepo wakati huo.

Kabla ya hapo nilitangazwa kama mhaini, wakati huo ninasoma mwaka wa kwanza wa theology (elimu ya dini). Kwa hiyo nilikuwa natafutwa na watawala kwa tuhuma za uhaini.

Kisa cha kutuhumiwa hivyo ni kuwa niliitisha mkutano wa wazazi mjini Arusha kujadili masuala ya wanafunzi wakati huo. Tulikuwa na Philip Marmo ambaye alikuwa anasoma Nairobi, Kenya

Mkutano ulikuwa ni wa kutafuta suluhu kwa mabinti ambao walikuwa wanakwenda kusoma form five (kidato cha tano) na six (sita), kuwapatia bweni maana walikuwa wanahangaika wakitoka vijijini.

Ilikuwa wakifika Arusha wanahangaika sana na wengine wanabakwa. Tukaitisha mkutano wa wazazi kutoka wilaya zote mbili; Karatu na Arusha, lakini wenzetu serikalini wakatafsiri vibaya wakidhani tunafanya siasa.

Mkutano wetu ukavamiwa na watu wenye suti,



kutoka mkoani, kuanzia RPC na wenzake.

Lakini tulifahamishwa mapema kuhusu hilo, lakini sisi hatukuogopa. Tukafanikiwa wazazi wakachanga hela tujenge mabweni na wao wakashindwa kutukamata.

Pambazuko: Nini kilikuwa kinakusukuma kufanya hayo yote licha ya hatari iliyokuwepo enzi zile?

Dkt. Slaa: Ni moyo wangu wa kutaka kuwasaidia watu. Sikuishia hapo. Baadaye tukafanya mkutano mwingine Karatu na lengo lilikuwa kuanzisha klabu za vijana.

Tukawa tunafuatiliwa na kufanyiwa ukachero, lakini tukabaini. Sisi kwenye mkutano tukaweka pombe, tukaweka na mabinti pale, tukijua kuwa wale askari watahangaika nao.

Tukafanikiwa.

Baada ya mkutano wetu usiku, mie nilikesha naandika minutes (kumbukumbu) za mkutano ili ziwasilishwe kwa mkuu wa wilaya asubuhi, nikafanikiwa.

Nikaandika andiko zuri tukianisha muundo wa vilabu za vijana, jinsi tutakavyopata fedha, jinsi vitakavyofanya uhamasishaji na mambo mengine, tukawasilisha.

Niliendelea na harakati hizi nikikumbana na mkuu wa wilaya akiitwa Leonard Mambo, akataka kutuweka ndani, lakini sjsi tulikuwa wasomi kuliko yeye.

Katika moja ya mikutano, ambayo alipanga kutukamata, asubuhi yake tulikwenda ofisini kwake tukamwambia mbele ya hadhara ya watu atuambie kama yeye ni wa Nyerere au si wa Nyerere?

Maana sisi tulikuwa tunafanya kazi ya Mwalimu Nyerere, lakini yeye anazipinga.

Wakati huo tulitaka atuandikie waraka wa kuturuhusu tufanye kazi ya kuhamasisha vijana, lakini

Inaendelea Uk. 23

Kampeni ya nishati safi yafikishwa Kizimkazi

Nestory BIZIRA na Kelvin SEBASTIAN

KAMPENI ya matumizi ya nishati safi ni moja na mambo yaliyofanyika katika Tamasha la Kizimkazi, lililohitimishwa hivi karibuni.

Tamasha hilo ambalo hufanyika kila mwaka katika kijiji cha Kizimkazi, Wilaya ya Kusini, Mkoa wa Kusini, Zanzibar alikozaliwa Rais Samia Suluhu Hassan, huwaleta pamoja watu kutoka kada mbalimbali na linahusisha nambo mbalimbali ikiwamo maonyesho, michezo, burudani, na makongamano yanayojadili mada mbalimbali.

Moja ya shughuli za tamasha hilo mwaka huu, Wizara ya Nishati, pamoja na taasisi zake, walishiriki kwa kufanya maonyesho na kongamano kuhusiana na umuhimu wa kutumia nishati safi na salama.

Kupitia tamasha hilo, watendaji wa wizara hiyo na taasisi zake, walielezea hatua zilizofikiwa katika utekelezaji wa Sera ya Nishati ya mwaka 2015.

Walitoa elimu kwa wananchi kuhusu utekelezaji wa mkakati wa taifa wa matumizi ya nishati safi ya kupikia.

Akizungumza katika kongamano hilo, Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Dkt. Doto Biteko, alisistiza kuwa matumizi ya nishati safi, ni muhimu kwa maendeleo ya nchi na utunzaji wa mazingira.

“Zaidi ya watu bilioni 2.4 hawatumii nishati safi, na kati ya hao watu milioni 933 wanatoka Afrika. Pia baadhi ya matendo maovu yanatokana na utumiaji wa nishati zisizokuwa safi na takribani watu milioni 3.7 hupoteza maisha kutokana na utumiaji ya nishati zisizokuwa safi,” alisema.

Dkt. Biteko alibainisha kuwa athari za utumiaji wa nishati zisizokuwa safi hutokea taratibu tofauti na magonjwa ya mlipuko kama kipindupindu au magonjwa mengine.



Banda la Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC) wananchi wameweza kujionea moja kwa moja shughuli za uchimbaji wa gesi asilia, usafirishaji na uchakataji wake kupitia teknolojia ya uhalisia pepe ‘Virtual Reality’. (Picha na HabariLeo)

Alisema suala la nishati safi limekuwa ajenda kubwa siyo Tanzania pekee, bali duniani kote kutokana na umuhimu wake katika maendeleo ya kisasa.

Alisema Tanzania imeonyesha kuunga mkono suala hili kwa vitendo kupitia kwa kampeni iliyoanzishwa na inayoendeshwa chini ya maelekezo ya Rais Samia.

Dkt. Biteko alisema matumizi ya nishati chafu yanawalazimisha watu kutumia muda mwingi kutafuta kuni au mkaa.

Akabainisha kuwa iwapo jamii zikiimarisha matumizi ya nishati safi, muda huo unaweza kutumika katika shughuli nyingine za maendeleo na kuleta mabadiliko makubwa katika jamii.

Aliwataka Watanzania mmoja mmoja na taasisi, kuunga mkono juhudi za Rais Samia katika jambo hilo ili kuifanya Tanzania kuwa kinara katika matumizi ya nishati safi na pia kuleta mabadiliko yatakayoboresha maisha ya watu.

Katika Banda la Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC), wananchi walishuhudia shughuli za uchimbaji wa gesi asilia, usafirishaji na uchakataji wake kupitia teknolojia ya ‘uhalisia - pepe’ pamoja na kuelezwa juhudi za serikali kuendeleza sekta ya mafuta na gesi asilia nchini.

Uchaguzi Marekani

Upekee mfumo wa uchaguzi Marekani



Makamu wa Rais wa Marekani, Kamala Harris

Na Mwandishi WETU

KUANZIA leo, gazeti lako la Pambazuko litakuletea uchambuzi wa kina kuhusiana na uchaguzi wa Marekani unaotarajiwa kufanyika Novemba 5, mwaka huu.

Hivi sasa kampeni zimepamba moto baada ya vyama vikubwa viwili; Democrat na Republican kuteua wagombea urais wao.

Kamala Harris, ambaye kwa sasa ni makamu wa rais, amepitishwa kwa mgombea urais kupitia chama cha Democrat, wakati Donald Trump, ambaye aliangushwa katika uchaguzi uliopita na rais wa sasa Joe Biden, amepitishwa kuwa mgombea wa Republican.

Ingawa jambo ambalo linagonga vichwa vya habari hivi sasa ni kampeni zinazoendelea, ni vyema tuanze kwa kuangalia taratibu za uchaguzi na mfumo wa uchaguzi nchini humo ili kuweka msingi wa uchambuzi wa mambo yatakayofuata.

Uchaguzi wa Rais

Uchaguzi wa Rais wa Marekani hufanyika kila baada ya miaka minne. Katika mwaka husika, uchaguzi hufanyika Jumanne ya kwanza ya mwezi Novemba.

Mtu anayetaka kuwania urais nchini humo anapaswa kuwa na umri usiopungua miaka 35, ambaye amezaliwa na ameishi Marekani katika kipindi cha miaka 14 iliyopita kabla ya kugombea.

Hii ni moja ya sababu iliyomfanya Trump kumpinga Barrack Obama wakati anagombea urais akidai kuwa mwanasiasa huyo hakuzaliwa Marekani.

Kwa kawaida, watu wanaotaka kuwania nafasi hiyo hutangaza nia zao takribani mwaka mmoja kabla ya uchaguzi.

Marekani hakuna tume ya kitaifa ya uchaguzi, hivyo uchaguzi husimamiwa na serikali za mitaa katika kila jimbo.

Lakini kunakuwa na maofisa mahsusi wanaoshughulikia na kuratibu uchaguzi nchi nzima.

Uteuzi

Baada ya wagombea kutangaza nia zao, mchakato wa uchaguzi huanza kwa kura za maoni kwa kila chama, ambapo wagomnbea urais huchuana katika majimbo na hatimaye katika mikutano mikuu ya vyama vyao ambavyo huteua wagombea.

Mikutano ya kampeni na kura za maoni huanza kati ya Januari na Februari katika mwaka wa uchaguzi na uteuzi wa mgombea unafanyika kabla ya kumalizika kwa mwezi Agosti.

Kura za maoni huandaliwa na matawi ya vyama katika majimbo husika na kura za siri zinatumika kuchuja wagombea.

Mchakato huu husaidia kuchuja wagombea kiasi kuwa inapofikia wakati wa mkutano mkuu wa uteuzi, kuna kuwa na wagiombea wachache tu wenye ushawishi ndio wanakuwa wamesalia katika kinyang'anyiro.

Wiki iliyopita Democrats walifanya mkutano kama huo na kumteua Harris kuwa mgombea wake. Kabla ya hapo, Joe Biden alitangaza kuwa atawania nafasi hiyo, lakini kutokana na matatizo yake ya kiafya yanayotokana na umri mkubwa, akakubali kuachia nafasi hiyo dakika za mwisho.

Kabla ya hapo, wanachama wa Republican walikuwa wamemteua Trump kuwa mgombea wao.

Kampeni

Inaendelea Uk. 17

Upekee mfumo wa uchaguzi Marekani

Inatoka Uk. 16

Kama sehemu ya kampeni, wagombea kutoka vyama vikubwa vya Democrats na Republican, hushiriki katika mdahalo kwa njia ya televisheni ambao huratibiwa na chombo huru.

Katika midahalo hiyo, maswali huandaliwa kwa kila mgombea kuhusu sera zake na pia kuhusu masuala muhimu ya nchi.

Hii husaidia kuonyesha tofauti ya misimamo baina ya wagombea hao kulingana na sera zao na za vyama vyao.

Mchakato wa uchaguzi

Uchaguzi wa Marekani una mchakato ambao unawachanganya watu wengi kwa sababu ni wa kipekee sana.

Tofauti na nchi nyingine, Rais wa Marekani hatokani na kura zinazopigwa na watu moja kwa moja, isipokuwa kura hizo zinatoa ushindi wa mgombea au chama kwenye jimbo husika na kila jimbo limepangiwa idadi mahsusi ya wawakilishi ambao ndio wanaotumika kumpata mshindi wa urais.

Kura hizo za uwakilishi huitwa 'electoral college' wakati zile zinazopigwa na wananchi huitwa 'popular votes.'

Hivyo, siyo ajabu kuwa na matokeo ambayo katika 'popular vote' mgombea anaweza kuwa amepata nyingi, lakini asichaguliwe kuwa rais kwa sababu hakupata idadi kubwa ya 'college votes.'

Hii hutokea pale mgombea anapopata 'popular votes' katika majimbo ambayo yana wapiga kura wa kawaida wengi, lakini yana idadi ndogo ya 'college votes.'

Tukumbuke kuwa kampeni za ndani za vyama za kutafuta wagombea na mchakato wa kura za maoni, uhesabika kama sehemu ya kampeni.

Hivyo, kimsingi, kampeni za uchaguzi wa Marekani huanza mwezi Januari na Februari pale kampeni za kura za maoni zinapoanza kwenye vyama kulingana na ratiba zao za kura za maoni.

Ingawa kura za maoni hufanyika katika majimbo mbalimbali, lakini ni matokeo ya majimbo ya Iowa, New Hampshire, Nevada na South Carolina ndiyo ambayo hutoa mgombea wa chama.

Haya ni majimbo ambayo yana ushawishi mkubwa katika siasa za Marekani, hivyo kinachoamuliwa na wananchi katika majimbo hayo kinakuwa na sauti kubwa.

Uchauzi wenyewe

Kama tulivyoona awali, wapiga kura hupiga kura katika majimbo yao, ingawa kura zao hazimchagui rais moja kwa moja.

Kila jimbo limepangiwa idadi ya 'electoral college votes' ambazo ndizo hutumika kumpata mshindi.

Kwa ujumla, kuna kura 538 za aina hii katika majimbo yote nchi nzima.

Na ili mgombea ahesabiwe kuwa mshindi, analazimika kupata zaidi ya nusu ya kura hizi.

Hivyo, mgombea anayepata 'electoral college votes' 270 anahesabiwa kuwa mshindi hata kama matokeo katika majimbo mengine hayajatangazwa.

Utaratibu huu unamaanisha kuwa wapiga kura wa kawaida wanapopiga kura huwachagua hawa wawakilishi ambao idadi yao ndiyo inatumika kumpata rais.

Utaratibu huu hutumika maeno yote Marekani, isipokuwa katika majimbo ya Maine na Nebraska.

Kuapishwa

Mtu anayechaguliwa kuwa Rais wa Marekani katika uchaguzi unaofanyika Jumanne ya kwanza ya Novemba katika mwaka wa uchaguzi, huapishwa Januari 20 ya mwaka unaofuata.

Wiki ijayo tutaanza kuangalia uchaguzi huo na jinsi kampeni zinavyoendelea, hasa baina ya wagombea wakubwa wawili; Kamala Harris na Donald Trump.



Donald Trump

Habari



Kaimu Katibu Tawala wa Mkoa wa Geita Dkt. Elfasi Msenya (katikati) akikata utepe kuashiria uzinduzi wa ofisi mpya ya tawi la benki ya MCB, mjini Geita mwishoni mwa wiki iliyopita. (Picha na Mpigapicha Wetu)

MCB yafungua tawi Geita, serikali yatia neno

Na Mwandishi WETU, Geita

SERIKALI Imezihimiza benki kote nchini kupanua wigo wa shughuli zao kwa kufungua matawi zaidi, hususan katika maeneo yenye fursa kubwa za kiuchumi.

Kufanya hivyo ni sehemu muhimu ya mkakati wa kuimarisha huduma za kifedha kwa biashara, ikiwa ni sehemu ya juhudi za Rais Samia Suluhu Hassan kujenga mazingira wezeshi na rafiki kwa biashara ili kuchochea ukuaji endelevu wa uchumi.

Dkt. Elfas Msenya, Kaimu Katibu Tawala wa Mkoa wa Geita, alitoa wito huu hivi karibuni katika hafla ya uzinduzi wa tawi jipya la Mwalimu Commercial Bank (MCB) mkoani humo.

Akizungumza kwenye hafla hiyo, Dkt. Msenya alisisitiza kuwa Geita ni eneo muhimu la kimkakati na kuwa ni kitovu cha shughuli za kiuchumi, hususan katika sekta za madini na biashara.

Alizihamasisha taasisi nyingine za kifedha kuiga mfano wa MCB kwa kufungua matawi katika mkoa huo ili kuleta huduma za kibenki karibu zaidi na wananchi, waliozungukwa na fursa lukuki.

"Uwepo wa MCB hapa Geita kutaongeza chachu na kutoa mchango mkubwa katika kukuza sekta ya kifedha na kuchangia ukuaji wa uchumi wa mkoa wetu," alisema Dkt. Msenya, akisisitiza kuwa mabadiliko chanya kwa uchumi wa eneo hilo, yanategemea sana uwepo wa sekta ya fedha.

Kwa upande wake, Ofisa Mtendaji Mkuu wa MCB, Richard Makungwa, alisema fursa nyingi za kiuchumi zilizomo mkoani Geita ndio sababu kubwa ya benki hiyo kufanya uamuzi a kufungua tawi hilo.

Alisema Mkoa wa Geita umejaaliwa fursa nyingi za kiuchumi na kibiashara kupitia sekta mbalimbali kama vile madini, kilimo na uvuvi.

Alisisitiza dhamira ya MCB ya kutoa huduma bora za kifedha zinazolenga kuvutia siyo tu wateja wadogo, bali pia wawekezaji.

Makungwa alisema huduma zitakazotolewa na benki hiyo kupitia tawi hilo zinalenga kuwasaidia wateja kuimarisha hali zao za kifedha na kuhakikisha kwamba MCB inabaki kuwa benki ya chaguo lao.

"Geita inajulikana kwa shughuli zake za uchimbaji madini, na tumejipanga kukidhi mahitaji ya kipekee ya sekta hii.

Dhamira yetu ni kutoa huduma bora kwa wateja wetu wote, huku tukilenga zaidi wale wanaojihusisha na madini.

Tuko hapa kusaidia kukua kwao na kujenga uhusiano wa kudumu nao," alisema Makungwa.

Pamoja na upanuzi wa huduma za kibenki, Kaimu Katibu Mkuu wa Chama cha Walimu Tanzania (CWT), Joseph Misalaba, alisisitiza umuhimu wa kwenda zaidi ya kufungua matawi mapya.

Tamisemi yapewa wiki moja kujibu hoja

Ni kesi ya kupinga uchaguzi serikali za mitaa



Bob Chacha Wangwe

Na Mwandishi WETU

MAHAKAMA Kuu ya Tanzania imeupa siku saba upande wa wajibu maombi kwenye shauri la kupinga Tamisemi kusimami uchaguzi wa serikali za mitaa

Kesi hiyo inayowahusisha Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi) pamoja na Mwanasheria Mkuu wa Serikali (AG), walipunguziwa siku moja, baada ya kuomba siku nane kwa ajii ya kuwasilisha majibu yao.

Akitoa uamuzi huo baada ya kusikiliza pande zote mbili, Jaji wa Mahakama Kuu anayesikiiza shauri hilo, Wilfred Dyansobora, alisema ombi la watoa majibu ambao ni mawakili wa serikali kutaka wapewe siku nane kuanzia Agosti 22, haliwezi kukubaliwa badala yake wanapewa siku saba, ili waweze kuwasilisha majibu yao baada ya kuwasiliana na wateja wao.

“Kwa hoja zilizotolewa na jinsi sheria zilivyokaa, mahakama imeridhika kuwa kwa kuwa mjibu maombi amekuja na amekuwa sehemu ya shauri hili, apewe nafasi...”

“Mahakama imeridhika kuwa siku saba kuanzia leo (Alhamisi Agosti 22) zinamtosha kufanya mawasiliano na kuleta majibu ili shauri hili liendelee kusikilizwa,” alisema Jaji Dyansobora.

Alisema kwa maana hiyo, katika shauri hilo lililowasilishwa mahakamani hapo na Bob Chacha Wangwe, Ananilea Nkya na Bubelwa Kaiza, wajibu maombi wanatakiwa kuwasilisha majibu yao ndani ya siku hizo saba kufikia mchana wa saa nane, Agosti 28, 2024 kabla kesi haijaanza kusikilizwa.

Jaji Dyansobora alitoa uamuzi huo baada ya upande wa mawakili wa serikali wakiongozwa na wakili Hanigi Hang’a kuwasilisha hati kinzani, wakiomba wapewe siku nane kwa ajili ya kuwasiliana na wateja wao na kupata majibu.

Uamuzi huo ulifikiwa baada ya awali, upande wa waleta maombi kupitia kwa wakili wao, Peter Madeleka, kupinga hoja ya kupewa siku nane na kutaka wapewe siku tatu kwa kuwa zinawatosha kufanya mawasiliano na wateja wao na kupata majibu.

Wakili Madeleka alikuwa akipinga ombi la upande wa wajibu maombi, baada ya kiongozi wa jopo la mawakili wa serikali, Hang-a kuieleza mahakama kuwa walipata maombi ya kuwasilisha majibu siku moja kabla, yaani Jumatano Agosti 21, hivyo hawajapata muda wa kuwasiliana na kuonana na wateja wao kwa kuwa wote wako Dodoma.

Hoja hiyo ya Madeleka ilipingwa vikali na wakili wa serikali, Eright Ruisha, ambaye aliiomba mahakama kuangalia vizuri kikwazo hicho, kwa kuwa japokuwa mahakama inaongozwa kwa sheria na kanuni, upande wa watoa majibu haujapewa muda wa kutosha, kwa kuwa japokuwa shauri hilo liliandaliwa Agosti 7, 2024 lilifikishwa mahakamani Agosti 21, ikiwa ni siku 14 baadaye.

Inaendelea Uk. 20

Haki

Tamisemi yapewa wiki moja kujibu hoja



Wakili Peter Madeleka

Inatoka Uk. 19

Alisema watoa maombi wametaka shauri hilo lisikilizwe kwa hati ya dharura ambapo sheria inaelekeza iwe ndani ya siku 14 tangu kuandaliwa kwa shauri hilo, hivyo kiufundi, kwa shauri hilo lililoandaliwa Agosti 7, 2024 lilitakiwa kwisha muda wake siku 14 baadaye, yaani Agosti 21, ambayo ndiyo siku lilipokelewa mahakamani na wajibu maombi kufikishiwa taarifa ya kuitwa mahakamani hapo.

"Sisi mawakili ni maofisa wa mahakama na kwa hiyo ni vyema tuishauri vizuri mahakama. Ni kweli shauri hili liliandaliwa Agosti 7, mwaka huu na hadi leo Agosti 22 ina maana siku 14 zimeisha jana, Agosti 21. Na leo ndiyo tuko hapa, ina maana kiufundi muda unaotajwa kisheria umeshaisha.

Tukichukua msimamo kuwa mahakama inaongozwa na sheria, kwa maana hiyo mahakama hii haitakuwa tena na uwezo wa kulisikiliza.

"Ili mahakama itoe haki, ni lazima pande zote mbili zipewe nafasi ya kusikilizwa. Katika mazingira hayo, tunatakiwa tutumie tafsiri ya kiufundi kwamba siku 14 zimeisha jana, jambo la kujiuliza ni kuwa je, tutakuwa tumefikia maamuzi yenye haki..?"

"Na sisi kama mawakili tutakuwa tumeisaidia mahakama? Ni ombi letu kuwa tupewe haki ya kusikilizwa," alisema.

Awali, kiongozi wa jopo la mawakili wa upande wa waleta maombi, Mpale Mpoki, alitaka ombi lolote litakalotolewa lihakikishe kuwa majibu yanawasilishwa kabla ya Agosti 28, 2024.

Hata hivyo, akitoa ufafanuzi kuhusu hoja za pande zote mbili kabla ya kutoa uamuzi, Jaji Dyansobora alisema mahakama haiwezi kukusudia siku 14 zinazoainishwa kwenye mashauri ya aina hiyo zianze siku ambayo shauri hilo lilitengenezwa, yaani Agosti 7, kwa kuwa kwa kufanya hivyo inamaanisha haitakuwa na uwezo wa kulisikiliza tena kwa sababu kisheria halitakuwepo tena.

Alisema hiyo inatokana na ukweli kwamba shauri hilo lilitengenezwa na kukaa mikononi mwa waombaji kwa siku saba kabla ya kuwasilishwa mahakamani, hivyo siku zitaanza kuhesabiwa siku ambayo yamepokelewa mahakamani.

Upande wa mashtaka uliwasilishwa na mawakili Mpale Mpoki na Peter Madeleka na upande wa serikali uliwakilishwa na mawakili Hanigi Hang'a, Eright Ruisha, Lilian Method, Ayubu Sanga na Luciana Kikala.

Katika kesi hiyo watoa maombi wametoa maombi matatu kwanza wakiitaka mahakama kutoa amri ya kufutwa kwa Sheria Ndogo zilizotolewa kupitia matangazo ya serikali namba. 571, 572, 573, na 574 ya Julai 12, 2024.

Pili wameiomba mahakama iape ruhusa kuwasilisha maombi ya kuizuia Tamisemi kuratibu, kuandaa na kusimamia uchaguzi wa serikali za mitaa wa mwaka 2024;

Na tatu wameitaka mahakama kuweka zuio kwa Tamisemi, mawakala wake, wawakilishi au wafanyakazi wake kuratibu, kuandaa, na kusimamia uchaguzi wa serikali za mitaa wa mwaka 2024.



Wanawake ‘wakamata’ idara za sheria Kenya

Na Julius MKAMBI, Nairobi

REBECCA Miano ndiye alikuwa chaguo la Rais wa Kenya William Ruto kuwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali, lakini baadaye alipewa majukumu mengine ya kuwa Waziri wa Utalii na Wanyamapori.

Laiti jina la Miano lingebaki kwa wadhifa aliyoteuliwa awali, angeweka historia ya kuwa mwanasheria mkuu wa kwanza mwanamke tangu Kenya kupata uhuru.

Hata hivyo, baadaye ya kuondoa jina la Rebecca Miano, Rais Ruto bado alifanya uteuzi wa mwanamke mwingine, Dorcas Oduor, kuchukua majukumu hayo ya kuwa mshauri wa serikali masuala ya kisheria. Mwanamama huyu kitaaluma ni mwanasheria.

Dorcas anajivunia uzoefu wa miaka 30 akihudumu katika Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka ya Umma akiwa Naibu Mkurugenzi wa Mashtaka ya Umma kabla ya kuapishwa kuwa Mwanasheria Mkuu wa Sheria baada ya kupitishwa na Bunge.

Sasa anakuwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali ya Kenya wa tisa tangu Kenya kupata uhuru mwaka 1963, watangulizi wake wakiwa Charles Njonjo (1963-1979), James Karugu (1980-1981), Joseph Kamere (1981-1983), Matthew Muli (1983-1991), Amos Wako (1991-2011), Githu Muigai (2011-2018), Paul Kihara Kariuki (2018-2022) na Justin Muturi (2022-2024).

Majukumu ya Dorcas anapoingia ofisini yatakuwa kutoa ushauri kwenye sera, uratibu na uangalizi kuhusiana na taasisi mbalimbali za sekta ya sheria na pia ndiye mtetezi wa utawala wa sheria na mtetezi wa maslahi ya umma.

Kupaa kwake kwenye ofisi hiyo kunafanya sekta ya haki kupiga hatua muhimu katika uwakilishi wa jinsia, hivyo Dorcas anaungana na wanawake wengine wanaoshikilia nyadhifa zenye nguvu katika sekta ya sheria.



Mwanasheria Mkuu wa Serikali ya Kenya, Dorcas Oduor

Yupo Jaji Mkuu Martha Koome ambaye pia yeye ni mwanamke wa kwanza kushikilia nyadhifa hiyo, huku Naibu Jaji Mkuu Msaidizi ni Philomena Mwilu na Msajili wa Mahakama ni Winfrida Mokaya Boyani.

Kwenye orodha ya wanawake wanaoshikilia vyeo vikubwa katika idara ya mahakama yumo Faith Odhiambo ambaye ni mwanamke wa kwanza kuchaguliwa Rais wa Chama cha Mawakili Kenya (LSK).

Wakati wa maandamano yaliyoitishwa na vijana wa Gen Z, Faith alikuwa mstari wa mbele kushinikiza Jeshi la Polisi kuwaachia Gen Z waliokamatwa au kutekwa kwenye maandamano ya kumtaka Rais Ruto kuwajibika.


Licha ya wanawake kukamata sehemu nyeti za idara ya sheria, nafasi ambazo bado hawajafanikiwa kupenya ni urais na unaibu rais, japo wapo wanawake walishawahi kugombea nafasi ya juu ya uongozi wa nchi.

Itakumbukwa kwenye uchaguzi mkuu uliyopita, takwimu zinaonyesha kuwa wagombea urais watatu kati ya wanne waliwachagua wanawake kuwa wagombea wenza.

Inaendelea Uk. 22

Kenya

Wanawake ‘wakamata’ idara...



Rais wa Kenya, Wiiliam Ruto akisalimiana na Mwanasheria Mkuu wa Serikali ya Kenya, Dorcas Oduor, Ikulu jijini Nairobi hivi karibuni. (Picha na The Star)

Inatoka Uk. 21

Rais Ruto alitoa uhakikisho wa kutimiza sheria ya jinsi ya thuluthi mbili kabla ya kutamatika kwa muhula wake ofisini.

“Ninataka kuwahakikishia wanawake wa Kenya kwamba safari hii tutatekeleza sheria ya jinsia ya thuluthi mbili,” alisema Rais Ruto.

Ruto alifichua kwamba amejitolea kuhakikisha kati ya maeneo bunge 290, angalau thuluthi moja ni wanawake na kuongeza atajadiliana na naibu wake, Rigathi Gachagua kuhusu mbinu zitakazoruhusu kujumuishwa kwa wanawake zaidi katika nyadhifa za uongozi.

Miongoni mwa mbinu hizo ni kukubaliana kwa pamoja kwamba endapo mgombea urais katika chama chao atakuwa mwanamume, basi mgombea mwenza awe mwanamke na kama mwanamke ndiyo atapeperusha bendera ya urais, mgombea mwenza atakuwa mwanamume.

Kauli ya Rais Ruto inakuja ikizingatiwa idadi ya magavana wanawake imeongezeka kutoka watatu kwenye uchaguzi mkuu wa mwaka 2017 hadi saba uchaguzi mkuu uliyopita. Magavana hao na kaunti wanazoziongoza kwenye mabano ni Gladys Wanga (Homabay), Ann Waiguru (Kirinyaga), Wavinya Ndeti (Machakos), Susan Kihika (Nakuru), Fatuma Achani (Kwale), Cecily Mbarire (Embu) na Kawira Mwangaza (Meru).

> **“Ninataka kuwahakikishia wanawake wa Kenya kwamba safari hii tutatekeleza sheria ya jinsia ya thuluthi mbili,” alisema Rais Ruto.**

Kati ya hao saba, Gavana Mwangaza anasubiri huruma za mahakama baada ya Bunge la Seneti kupiga kura ya kumuondoa uongozini.

Hata hivyo, miongoni mwa nchi za Afrika Mashariki, Kenya kwa sasa inashika nafasi ya chini zaidi katika uwakilishi wa jinsi ambapo kwenye bunge la 10, wanawake waliunda asilimia 9.8 pekee na idadi hiyo kupanda hadi kufika asilimia 20.7 kwenye bunge la 11.

Aliyewahi kuwa Jaji Mkuu wa Kenya, David Maraga, alimwandikia barua kiongozi wan chi wa wakati huo, Rais Uhuru Kenyatta akimtaka avunje Bunge kutokana na kushindwa kutekeleza Ibara 27(8) ya Katiba ya Kenya inayotaka wajumbe wa kuchaguliwa au kuteuliwa wasiwe zaidi ya theluthi mbili ya jinsi moja.

Ni agizo ambalo Kenyatta alilipuuza ila aliyekuwa naibu wake wakati huo, William Ruto, aliibeba kama moja ya ajenda zake kwenye kampeni kuelekea uchaguzi mkuu wa mwaka 2022, akiahidi kutekeleza ibara hiyo ya Katiba kwa vitendo.

Ruto alisema akichaguliwa rais wa awamu ya tano, baraza lake la mawaziri litajumuisha asilimia 50 ya wanawake na kuwaahidi kuwafanya washirika sawa katika serikali yake akisisitiza (wanawake) watakuwa sura ya utawala wa muungano wa Kenya Kwanza.

Hata hivyo, baraza lake la mawaziri ambalo alilazimika kulivunja lote kabla ya kuliteua upya, akijumuisha baadhi ya viongozi wa upinzani kufuatia shinikizo la vijana wa Gen Z, lilijumuisha wanawake saba likiwa ni pungufu ya wanawake wanne kutimiza asilimia 50.

Slaa: Tume Huru ya Uchaguzi kiini macho

Inatoka Uk. 14

akafanya hila akatunyima hiyo barua licha ya kutuahidi kuwa atatuandikia.

Baadaye katika masono yangu nikaenda Tabora. Nilipofika pale nikaenda mkoani na kuwaambia kuwa nataka kuanzisha program ya elimu ya watu wazima. Pendekezo langu likapelekwa kwenye kamati ya chama ya mkoa.

Nikaitwa kwenye kamati ya chama wakati nikiwa mwanafunzi wa mwaka wa kwanza wa Theology pale Kipalapala.

Wakasema wazo langu ni zuri na si tu kuwa wanalikubali, bali nikateuliwa kuwa ofisa elimu ya watu wazima wa mkoa, nikapewa na gari ambalo nilikuwa nalala nalo shuleni.

Nikafanya kazi hiyo kwa miaka minne. Niliporudi Karatu, mkuu wa wilaya bado aliendelea kuniwinda. Tukaandika barua kwa Rashid Kawawa, akatuita na mwenzangu twende Dar es Salaam kwa maana alifurahishwa na lile andiko letu la kuanzisha vilabu vya vijana na akaamuru kuwa gari la mkuu wa wilaya ndilo litupeleke.

Baada ya hapo nikachaguliwa kuwa katibu wa tawi la chama katika kata yetu ya Seminari Kipalapala, Tabora. Ofisi yangu ilikuwa kwenye nyumba ya Chifu Fundikira.

Kwa hiyo mimi nilianza kufanya kazi za serikali nikiwa mwanafunzi. Kwa hiyo mimi siasa sikuanza kama masihara, nimeanza na misukosuko. Sasa ukitaka kunitafsiri kisiasa, inabidi ujue historia yangu hiyo.

Nilianza kama mtetezi wa watu bila kujali itikadi zao na ndio ambalo ninataka kulifanya hivi sasa kama mshauri huru, kuwashauri watu wote bila kujali itikadi zao kisiasa.

Wakati nilipoenda kusoma Italia mwaka 1979 nikateuliwa kupitia ubalozi kuwa katibu wa shina la pale.

Unamkumbuka Ally Sykes, alikuwa balozi wetu wakati huo alifukuzwa na Mwalimu Nyerere ubalozini na chanzo ni mimi. Mimi ndiye nilikuwa nampokea Mwalimu kila akija.

Pambazuko: Kwa hiyo uliendelea kuwa mwanachama wa siasa wakati ulipokuwa unafanya kazi kanisani?

Dkt. Slaa: Niliporudi nikiwa padre, kwa kuwa siruhusiwi kufanya kazi ya siasa nilirudisha kadi yangu ya CCM.

Nikafanya kazi yangu hadi kufikia nafasi ya Katibu wa TEC.

Mwaka 1995, wananchi wa Karatu walipokuja kuniomba nigombee ubunge ndio nikarudi tena kwenye siasa.

Walikuja kuniomba maji, walitaka maji. Nikawaambia nitakuja kuwasaidia kupata maji, lakini wao wakataka niwe mbunge kabisa.

Nikaenda kufanya tathmini, nikasisitiza kuwa nitawasaidia kupata maji, lakini wao wakalazimisha niwe mbunge.

Wakati huo kila chama kilikuwa kina mgombea wake tayari, lakini watu wakaja wakaniomba na mimi nigombee. Nikawaambia mimi chama changu CCM na tayari kimeshapata mtu. Wakaniambia chama chochote utakachogombea tutakuchagua.

Nikaomba kupitia CCM, lakini jina langu likakatwa. Sumaye akataka kuniunganisha na Rais Mkapa, wakati huo akiwa ndiye mwenyekiti wa CCM, ili jina langu lirudishe, lakini nikakataa.

Walipokuwa Dodoma kwenye vikao vya juu vya chama, Sumaye akanipigia tena akaniambia Mkapa amejazwa maneno ya uongo, njoo tuzungumze naye. Nikatakataa. Wakamteua Qorro kugombea.

Pambazuko: Hapo ndipo ulipokwenda Chadema?

Dkt. Slaa: Sikwenda moja kwa moja. Baada ya kushindwa kwenye uteuzi nikaamua kuachana na siasa nikarudi Dar es Salaam.

Wananchi wa Karatu wakatoka na basi la watu 60 kuja Dar es Salaam kunishawishi nigombee na wameshajaza fomu tayari.

Kwa kuwa vyama vyote vikubwa vilikuwa vimeshajaza watu, kilichokuwa kimesalia ni chama kidogo wakati ule ambacho kilikuwa hakijulikani sana, Chadema.

Nikawasikiliza, lakini sikuwajibu moja kwa moja. Nikawaomba wanipe muda, wakaondoka kwenda kupumzika.

Usiku nikaanza kuwauliza watu. Mmoja niliyemuuliza ni wakili Maira ambaye alikuwa jirani yangu.

Inaendelea Uk. 27

Mtoto wa Mvuvi



Na Maregesi PAUL

Nawaona waliohamishiwa Msomera wakirudi kuishi kwao Ngorongoro



Mkazi wa Msomera akiwa nje ya nyumba walizojengewa na serikali. (Picha na Mtandao)

NIMEAMBIWA kuwa tofauti zilizokuwapo kati ya wananchi wa Tarafa ya Ngorongoro na serikali, zimemalizika kwa amani.

Tofauti hizo hazikumalizika kwa sababu wananchi wa Ngorongoro waliamua kuzimaliza, hazikufikia mwisho kwa sababu viongozi wa wilaya yao waliamua kuzitatua, ila tofauti hizo baada ya Rais Samia Suluhu Hassan, kuruhusu wananchi hao waendelee kuishi katika makazi yao huku huduma za jamii zilizokuwa zimesitishwa zikirudishwa.

Sipendi kuingia kwa undani kujua nani aliamuru huduma hizo za jamii kama maji, afya, elimu na nyinginezo nyingi, ziondolewe kwa wakazi wa tarafa hiyo, ila kwa sasa ieleweke kwamba, Rais Samia ameagiza huduma hizo zirudishwe.

Hilo ni jambo jema na nina kila sababu ya kumpongeza Rais Samia kwa uamuzi huo, kwani unaonyesha ni kwa kiasi gani anavyojali maisha ya Watanzania.

Kwa hiyo, sasa tuchape kazi, askari polisi waliokuwa Ngorogoro wakidaiwa kutokea katika maeneo mbalimbali ya Mkoa wa Arusha na Manyara, warudi katika vituo vyao vya kazi na wengine wote waliokuwa Ngorongoro kwa kazi maalum, naamini wanajua kwamba sasa hali ni shwari Ngorongoro na wao sasa warejee kwenye kituo vituo vyao vya kazi.

Askari wa wanyamapori walioacha majukumu yao ya kuwalinda viumbe hao wasidhuriwe na majangili, warudi katika majukumu yao ya kila siku na watumishi wa serikali waliokuwa na kazi za dharura Ngorongoro ili kuhakikisha usalama unakuwapo mahali hapo, waondoke.

Hawa wote waondoke kwa kuwa Wamasai wameruhusiwa kuendelea na shughuli zao za kila siku.

Hofu yangu sasa ni moja tu, kwamba kuna uwezekano Wamasai waliohamia Msomera, Wilaya ya Handeni, Tanga, kwa hiari yao wakitokea Ngorongoro, wanaweza kurudi tena walikokuwa awali kwa sababu serikali imehalalisha wenzao waendelee kuishi katika eneo hilo.

Ninahofia hivyo kwa sababu kama wananchi hao walihamia Msomera kwa shingo upande, wakihofia uamuzi wowote mbaya unaoweza kutolewa pindi watakapogoma kwenda kwenye makazi mapya Msomera, sasa wanaweza kurudi Ngorongoro kwa sababu Rais ameruhusu wenzao waendelee kuwapo.

Hivyo basi, ili wananchi hao wasiwe na mpango mwingine wa kurudi Ngorogoro, kuna haja kwa serikali kuhakikisha mazingira ya Msomera yanaendelea kuwa mazuri zaidi kuliko Ngorongoro, ili kuwafanya wakazi wa eneo hilo wasiifikirie tena Ngorongoro ambako ndiko walikozaliwa na kukulia.

Mazingira ya ufugaji Msomera yaangaliwe kwa jicho la pekee, shule zote zilizoko katika eneo hilo ziwe na walimu wa kutosha, vitabu vya kutosha na hali kadhalika upatikanaji wa vyakula, huduma za afya, maji, barabara na nyinginezo zipewe kipaumbele ili wananchi hao wajione wako Ngorongoro ingawa wanaishi Msomera.

Afya

Unyanyapaa tishio kwa wenye kifafa

Na Arodia PETER

KIFAFA ni ugonjwa sugu wa neva unaotokana na mtu kupata mshituko katika ubongo na kusababisha degedege au kuanguka.

Hali hii hutofautiana kutoka mtu mmoja hadi mwingine kulingana na ukubwa wa mshituko.


Kwa mujibu wa Shirika la Afya Duniani (WHO), kifafa ni moja ya hali kongwe zaidi duniani inayotambulika, ikiwa na rekodi zilizoandikwa tangu miaka 4,000 kabla ya kuzaliwa Kristo.

Ugonja huu husababishwa na kuzalishwa kwa umeme mwingi kupita kiasi katika kundi la seli za ubongo.

Tafiti za kisayansi zinaeleza kuwa sehemu mbalimbali za ubongo zinaweza kuwa chanzo cha utoaji umeme huo wa mwili usiokuwa wa kawaida.

Mshituko hutofautiana kutoka muda mfupi zaidi au mshtuko wa misuli hadi degedege kali ya muda mrefu. Mshtuko pia unaweza kutofautiana mzunguko kutoka chini ya mshituko mmoja kwa mwaka hadi mara kadhaa kwa siku.

Hata hivyo, mtu kupata degedege mara moja, haimaanishi kuwa ana kifafa, kwani asilimia 10 ya watu duniani wamewahi kupata degedege mara moja katika maisha yao.



Katibu Mkuu wa Chama cha Wazazi wa Watoto wanaoishi na Maradhi ya Kifafa Tanzania (Uwakita), Judith Kivugo, akizungumza na waandishi wa habari hivi karibuni jijini Dar es Salaam. (Na Mpigapicha wetu)

Kama ilivyo kwa mataifa mengine, Tanzania pia ni miongoni mwa nchi zenye watu wanaougua ugonjwa huo wa kifafa.

Chama cha wazazi wa watoto wanaoishi na kifafa (Uwakita) pamoja na wadau wengine, walikutana jijini Dar es Salaam hivi karibuni kuweka mikakati ya pamoja juu ya kuukabili ugonjwa huo.

Katika mjadala huo, mambo kadhaa yalijitokeza, lakini unyanyapaa ulielezwa kuwa ni hatari na kikwazo kwenye suala zima la matibabu ya watu wanaoishi na ukifafa.

Daktari bingwa wa afya na magonjwa ya akili wa Hospitali ya Taifa Muhimbili – Upanga, Dar es Salaam, Nurueri Kitomary, anasema zaidi ya watu milioni 50 duniani wanaishi na hali ya ukifafa ambapo asilimia 80 wanaishi kwenye nchi zenye hali duni, nyigi zikwia barani Afrika na Tanzania ikiwemo.

Anasema watu milioni 10 wanaishi Afrika na hali ya ukifafa, na kwamba kuna uwezekano idadi hiyo imeongezeka hivi sasa kwa sababu takwimu hizo ni za zamani kidogo.

Dkt. Kitomari anasema mwaka 2022, WHO iligundua kuwa watu 45,000 nchini Tanzania wanaishi na hali ya ukifafa.

Na kwamba idadi hiyo ni kwa wale tu wanaofika hospitali kutafuta matibabu hospitalini, lakini kuna kundi kubwa nje ya hao wanaoendelea kufichwa majumbani na wengine kutibiwa kwa waganga wa kienyeji na maeneo mengine kama kuombewa makanisani.

“Unaweza kuona kuna namba kubwa ya hawa ambao hatuwajui. Yaani ni asilimia 3.7 tu ndio wapo kwenye matibabu, hivyo, bado tuna kazi kubwa ya kufanya ili watu zaidi ya asilimia 96 waingie kwenye mfumo.

“Ni vizuri jamii ifahamu kuwa magonjwa haya yanaongoza kwa kuleta ulemavu, kwa sababu wengi wanaofungiwa ndani, wanashindwa kujishughulisha na shughuli za kijamii na kuzalisha kipato kwa sababu ya unyanyapaa, ambayo hakika ni dhana potofu, ” anasema Dkt. Kitomari.

Inaendelea Uk. 26

Afya

Unyanyapaa tishio kwa wenye kifafa

Inatoka Uk. 25

Bingwa huyo wa tiba anasema; “unyanyapaa ni moja ya kizuizi kikubwa cha shughuli zote za kumtibu mtu anayeishi na hali ya ukifafa...”

“Mwingine anajinyanyapaa mwenyewe kwa sababu ya malezi na makuzi kwenye jamii yake inayomuona mgonjwa wa kifaa kuwa ni mtu mwenye ‘mapepo’, bahati mbaya, mkosi na majina mengine mabaya,” anasema.

Mratibu wa Afya ya Akili Manispaa ya Kinondoni, Dkt. Mwendo Peter, anasema mapambano dhidi ya maradhi hayo yanakabiliwa na changamoto kubwa ya unyanyapaa kwa watu wanaougua ugonjwa huo, jambo ambalo anasema linahitaji kampeni kubwa ya utoaji elimu kwa jamii.

Anasema unyanyapaa huo mkubwa umechangiwa na masuala mtambuka, zikiwamo mila, desturi na tamaduni tangu zamani ambapo familia zilizokuwa na mtu anayeishi na kifafa zilikuwa zinatengwa.

“Hili jambo lina historia kutoka kwa mababu zetu, kwamba mtu hawezi kuoa kwenye familia ambayo ina watu au mtu anayeugua kifafa; vitu hivyo vimeendelea hadi sasa na hivyo kupoteza watu na wataalam wenye uwezo mzuri kutumikia jamii kama watu wengine,” anasema.

Anaongeza; “kutokana na unyanyapaa huo, baadhi ya wagonjwa wanaamua kujinyanyapaa wenyewe kwa kutokwenda hospitali na ndugu zao; mwingine anakuja kituo cha afya kwa kujificha ili watu wasimuone. Mtu wa aina hii hawezi kusikiliza sawa sawa ushauri na maelekezo ya daktari au mshauri wa ustawi wa jamii kuhusiana na maradhi yake.”

Kutokana na hali hiyo, Dkt. Peter anasema mgonjwa wa namna hiyo hata akipewa dawa, haiwezi kumsaidia kwani anaweza kufika nyumbani asizitumie kwa usahihi.

Aidha, daktari huyo anashauri watumishi wanaowahudumia wagonjwa wanaoishi na ukifafa wapatiwe elimu ya ziada ili kuendana na mazingira ya sasa ya maendeleo ya teknolojia inayokwenda kwa kasi sana duniani.

Anasema asilimia kubwa ya watumishi katika vituo vya afya na hospitali wanatumia mbinu na elimu waliyoisoma darasani tu ambayo kwa sasa haitoshi. Anasema wanahitaji kuongezewa ujuzi wa mara kwa mara ili waweze kuendana na wakati.

“Utaalam wetu umepitwa na wakati, kile tulichojifunza darasani miaka mingi iliyopita, ni kilekile, hatuna cha ziada. Hivyo litakuwa jambo la msingi watalaam wetu wakaongezewa ujuzi kupitia mafunzo mbalimbali,” anasisitiza.

Kuhusu kupatikana dawa kwa watu wanaoishi na ukifafa, Dkt. Peter anasema ni changamoto nyingine inayopaswa kuangaliwa vyema.

Anatolea mfano kwamba katika Jiji la Dar es Salaam, dawa kwa ajili ya watu wenye kifafa zipo, lakini upatikanaji wake ni changamoto kwa sababu zinalipiwa.

“Kama mnavyojua, asilimia kubwa ya watu wenye changamoto ya ugonjwa huo uwezo wao kiuchumi, hivyo kushindwa kumudu kumudu gharama hizo,” anasema.

Mmoja wa wazazi mwenye mtoto anayeishi na changamoto ya kifafa, Jovina Josephati Hamis, anasema unyanyapaa unarudisha nyuma juhudi za matibabu ya ugonjwa huo nchini.

Anatolea mfano madaktari katika hospitali moja (jina linahifadhiwa) waliompima mtoto wake na kugundua tatizo hilo kwa mara ya kwanza, lakini hawakujali kumpa elimu zaidi wala kumshauri afanye nini.

“Naweza kusema daktari wa hospitali ya ..(anaitaja) nilipofanya kipimo, daktari alikuja moja kwa moja ananiambia mtoto wangu ana ugonjwa wa kifafa. Nilimwomba anielezee vizuri, lakini hakujali, aliniacha kwenye benchi la hosptali.

“Nilipoteza mwelekeo na kusahau mlango wa kurudi nilipotoka. Alipaswa kuniandaa kisaikolojia, kunielimisha ili nipokee hayo majibu kwa utulivu. Je, tunao madaktari wangapi wa aina hiyo? Je, wameandaliwaje kuelimisha wateja wao ambao ni wazazi au wagonjwa wenyewe?” Anahoji.

Slaa: Tume Huru...

Inatoka Uk. 23

Akanimbia kama wamekufuata kutoka kijijini kuja kukuomba ugombee, nenda.

Sikuridhika na Maira, lakini nikaanza safari ya Karatu. Wakati nakwenda nikapita Monduli kwa Lowassa.

Lowassa ni rafiki yangu wa siku nyingi sana. Nimejenga CBRT kupitia Lowassa, ndiye aliyenipa ardhi pale kwa nguvu. Aliimega ile ardhi kutoka Tirdo, akalazimisha.

Yeye mwenyewe akashtakiwa. Wakati huo alikuwa ametafuta ardhi Segerea, Salasala akashindwa ndio akapata pale.

Nilipofika kwa Lowassa nilimkuta ameshaanza kampeni za chini chini. Nikamwambia habari zangu akaniambia kama watu wa Karatu wamekufuata, nenda.

Baadaye Lowassa, katikati ya kampeni alitumwa na Mkapa kuja kunibomoa, hakuja. Alikataa. Alisema siwezi kwenda kumbomoa rafiki yangu. Hakuja.

Pambazuko: Vipi sasa watu au vyama vimeanza kuja kwako kuomba ushauri?

Dkt. Slaa: Baada ya kutoka Chadema nilisema sina chama, yeyote anayehitaji ushauri wangu nitampa, mwenye ajenda nzuri ambaye anataka kuiboresha aje.

Nina vyama zaidi ya 10 katiba zao zipo kwangu wananiomba ushauri, lakini sasa hivi wameacha kuja, nimeshawatupilia mbali kwa sababu nimeona hawana maana.

Nimewatupilia mbali kikiwamo chama kimoja mnachodhani kuwa ni kikubwa kwa sababu katiba yao ni ya hovyo.

Pambazuko: Sasa hivi wakazi wa Karatu wakija kukuomba utakwenda kugombea?

Dkt. Slaa: Wameshakuja sana hapa kuniomba nimewakatalia kugombea, lakini nimewaahidi nitawasaidia.

Mwezi wa tisa nitakwenda huko kuwasaidia, lakini siwezi kugombea tena. Wanao vijana wazuri wanagombea, nitakwenda kuwasaidia.

Wapo vijana wawili wazuri na wote ni vijana wangu.

Mmoja ni kijana mzuri sana anagombea kupitia Chadema na mwingine ni kijana wa mdogo wangu kabisa.

Nimewaambia wamalize uteuzi kwanza wakishampata mgombea nitakwenda kumsaidia. Sitaki kuingilia uteuzi kwa sababu vijana wote wananihusu kwa karibu.

Pambazuko: Unaonaje mabadiliko ya hivi karibuni ya sheria iliyozaa Tume Huru ya Uchaguzi?

Dkt. Slaa: Hakuna mabadiliko, kuna kaburi. Jambo lililopo kwenye Katiba hauwezi kulifanyia mabadiliko bila kurekebisha Katiba kwanza.

Mwanasheria yeyote anajua, jambo lililowekwa na Katiba huwezi kubadilisha kitu kwenye sheria bila kufanyia mabadiliko Katiba. Wao ndivyo walivyofanya.

Hauwezi kuwa na Tume Huru ya Uchaguzi kwa maneno tu. Kuna misingi minne ambayo ndio inaifanya tume yoyote kuwa huru, sio jina.

Hatuwezi kukuita wewe kuwa ni mwema kwa kuangalia uso, tunaangalia moyo wako.

Na kwenye Katiba hakuna neno Tume Huru.

Duniani kote, Tume inakuwa huru kwa vitu nikubwa vinne; cha kwanza, nani anamteua nani. Walichofanya sasa wameingiza kitu kinaitwa kamati ya usaili. Lakini hii kamati inaundwa na nani? Inaundwa na Jaji Mkuu wa Tanzania. Nani anamteua Jaji Mkuu wa Tanzania, wa Zanzibar? Nani anamteau mwenyekiti wa Kamati ya Maadili? Sasa utategemeaje uhuru wa Tume pale.

Kitu cha pili, tume inajulikana kuwa ni independent (huru) ikiwa na financial independency (uhuru wa kifedha). Tume yetu inategemea bajeti kutoka Ofisi ya Waziri Mkuu. Kwa hiyo mwenyekiti wa tume anapiga magoti kwa Majaliwa (Waziri Mkuu)? Halafu mtegemee kuwa itakuwa huru.

Halafu kitu cha tatu, security of tenure (usalama wa ajira). Anayeongoza tume na wenzake wana uhakika wa ajira zao? Rais Samia hajamwita jaji akamwondoa mahakamani akampelea kuwa mshauri wake ofisini? Mwingine amemtoa pale amempeleka kuwa Mwanasheria Mkuu, Feleshi si alikuwa pale.

Kitu kingine cha nne, muhimu sana ni mamlaka inayosimamia. Tume inaundwa na majaji kama viongozi wake wa juu. Majaji wanasimamiwa na chombo cha serikali, unapoataje uhuru wa tume?

Tulipotaka tuwe na tume huru tulitaka iwe huru kwa kuitengenezea bajeti mahsusi. Kuwe na kiwango kinachojulikana cha bajeti ya tume na kuwe na mfuko maalum kama ulivyo mfuko wa Bunge. Na serikali ihakikishe kuwa inapeleka fedha zote zilizotengwa kwa ajili ya Tume.

Itaendelea...

Riwaya

Viaticum-3

Sakramenti ya Mwisho



Paka analamba maziwa

Na Mchungaji Godwin Chilewa, Texas. Marekani

WIKI iliyopita tuliona namna gazeti la Mizani lilivyoanza kupata umaarufu na kurejesha heshima yake, kiasi kwamba waandishi wengi wakaomba kujiunga nalo, je, nini kitafuata?

Endelea sehemu hii ya tatu...

Ni kwa sababu hii Eddy huwiwa kumheshimu binti huyu kipekee na kumchukulia kama dada yake wa tumbo moja japokuwa mara nyingine binti wa watu huonesha dalili za kutaka kuvuka mipaka.

Pamoja na kukubaliana na ile nahau ya Kiswahili isemayo 'paka huwa hakatai maziwa' - kwa binti huyu, Eddy akajikuta akijifunga kidhibiti mwendo, asiharibu kazi.

"Kuna ile kesi ya Makhan, yule mfanyabiashara mwenye asili ya Kihindi anayetuhumiwa kuua familia yake yote na kujaribu kujiua kwa kujipiga risasi. Je! umepata lolote kutoka kwa kile chanzo chetu? Eddy alimuuliza Stella huku akimkazia macho.

"Amesema ataileta leo kwani ameshakamilisha kila kitu. Kama ujuavyo yule bwana huwa haamini mtu mwingine isipokuwa wewe. Lakini nilipoongea naye alinidokeza kwamba anao ushahidi wa kutosha kuthibitisha kuwa Makhani hakufanya yale mauaji, bali amebambikizwa hii kesi kwa sababu asizozijua..."

"Mh! Ana ushahidi wa kutosha? Maana hii kesi ni ngumu mno, amesema amepata mkanda wa video unaoonesha kila kitu.."

"Ni mkanda wa video uliorekodiwa na mtu au kamera ya usalama?"

"Sina hakika, lakini kwa jinsi maelezo yake yalivyokuwa, inaelekea kuna mtu aliyerekodi tukio hilo kwa simu ya mkononi..."

"Sijui huyo mtu ni nani, alikuwa wapi, na ilikuwaje hata akaweza kurekodi tukio la kutisha vile. Maana anadai tukio lote, kutoka mwanzo hadi mwisho, limo kwenye klipu ya video hiyo"

"Safi sana. Vipi John naye, amefikia wapi? Sikutaka kuuliza habari zake kwenye postmortem maana hakuwepo"

"Amefuatilia taarifa ya yule kanali wa jeshi anayetuhumiwa kushirikiana na mabwana wa vita kuuza silaha kwa wapinzani wa serikali ya Kongo"

"Vizuri sana" Eddy alijibu akiwa nimeridhishwa na maelezo ya Stella. Basi akachukua kisu cha mpingo, akafungua bahasha aliyopewa.

Wakati akifanya hivyo, ghafla ukasikika mlipuko mkubwa uliotingisha jengo zima huku ukienda sambamba na kukatika kwa umeme.

"Vipi tena?" Eddy aliuliza kwa mshituko kidogo.

"Usishituke bosi, ni hilo transfoma la umeme hapo nje limelipuka tena. Sisi tumeshalizoea! Leo ni mara ya nne katika kipindi cha wiki mbili linalipuka kwa kishindo na kukata umeme"

"Wenyewe wana habari?

"Wanayo habari. Kila likilipuka huwa wanakuja kulichokonoa mpaka linatengemaa, lakini baada ya siku mbili au tatu linalipuka tena. Cha ajabu transfoma lenyewe ni jipya, lilifungwa miezi michache tu iliyopita, kipindi ulipokuwa safarini Singapore."

"Ukiona hivyo afisa maduhuli aliyelinunua amejenga Mbezi Beach kama siyo Oystebay"

"Ndiyo Tanzania yetu" Stella lisema huku akitingisha kichwa kwa masikitiko.

Maneno hayo yalimuingia Eddy moyoni kama

Inaendelea Uk. 29

Viaticum-3

Sakramenti ya Mwisho

Inatoka Uk. 28

mwiba maana yalijaa ukweli usiopingika. "Inasikitisha kuona hata baada ya nusu karne ya kujitawala bado watu wetu hawatambui na kuthamini maana ya uhuru kamili.

Wengi wanajali kujaza matumbo yao na familia zao bila kufikiria uhai na maslahi ya watu wengine" alifikiria.

Mawazo hayo yalimfanya aende mbali zaidi, miaka ya 1970 wakati marehemu Edward Mondrane alipouawa kwa bomu la barua lililotumwa na majasusi wa Kireno.

Akajiuliza, hivi Msumbiji ingekuwaje leo hii kama Mondrane na Samora Machel wangekuwa bado wakiishi? Hakika Afrika imepoteza mashujaa wengi sana! Alijiambia.

Wakati Stella akinyanyuka kufungua madirisha ya vioo kuruhusu hewa iingie ndani, taa na viyoyozi vikawaka.

Mafundi wa Mizani walikuwa wameshawasha jenereta ya umeme. Eddy akatabasamu kwa furaha. Watu wake walikuwa hodari, waaminifu, wazalendo na wenye moyo wa kujituma hasa.

Ndani ya bahasha kulikuwa na tiketi moja ya Shirika la Ndege la Tanzania (ATC) inayofaa kusafiria kutoka Dar es Salaam kwenda Mwanza na kurudi.

Iliandikwa jina Eddy Kashe. Kwa jinsi tiketi yenyewe ilivyokuwa ilionesha wazi kwamba ilinunuliwa mtandaoni, kwenye 'website' ya Air Tanzania na kuchapwa kwenye karatasi ya kawaida. Jambo hili lilimshangaza kidogo, kwani hakuwa amepanga kwenda Mwanza.

Pamoja na tiketi hiyo, ndani ya bahasha kulikuwa na karatasi nyingine nzito, ya rangi ya maziwa iliyokunjwa vizuri kuhifadhi nyaraka nyingine ndani yake.

Akaifungua taratibu kuona kilichomo. Akashituka kuona kumbe ni fedha za kigeni, dola mia mia za Marekani.

Akainua macho kumtazama Stella aliyekuwa ameketi mbele yake. Macho yao yakagongana maana naye alikuwa akimuangalia kwa mshangao.

Kuona hivyo hakusema neno, akazitoa zile fedha, akaziweka juu ya meza, pembeni ya bahasha, akaelekeza macho yake kwenye ujumbe ulioandikwa kwenye karatasi iliyotumika kufungia fedha.

Ulikuwa ujumbe mfupi ulioandikwa kwa kalamu ya wino mwekundu:

"Eddy, hudhuria misa ya watakatifu wote itakayofanyika Siku ya Ijumaa tarehe moja, Novemba saa moja kamili asubuhi, kwenye Kanisa Kuu la Epifania, Bugando Mwanza. Usikose"

Kwa sekunde kadhaa, Eddy alibaki ameduwaa, akiukodolea macho ujumbe ule kana kwamba ulikuwa haueleweki.

"Vipi bosi, mbona umepigwa na butwaa?" Stella aliuliza baada ya kumuona akiendelea kuikodolea macho karatasi ile bila kusema lolote.

Eddy hakumjibu, akanyoosha mkono kumpa ile karatasi ili ajisomee mwenyewe. Stella akaipokea na kuisoma kwa makini.

"Bosi, mbona ujumbe wenyewe unaeleweka? Aliuliza kwa mshangao huku akimrudishia karatasi hiyo.

"Unaeleweka vipi wakati hauna jina kamili, anuani ya mwandishi, wala sababu za kunifanya niache shughuli zangu kwenda Mwanza?

"Uko sahihi bosi, hata hivyo hilo haliondoi ukweli kwamba yaliyomo humo yanajitosheleza."

"Una maana gani?"

"Ujumbe huu unakutaka uhudhurie misa ya watakatifu wote inayofanyika mjini Mwanza tarehe moja Novemba ambayo ni kesho kutwa..."

"Hili halina mjadala kwani kila tarehe moja ya mwezi Novemba Kanisa Katoliki huadhimisha siku ya watakatifu wote duniani. Kwahiyo uwepo wa misa hiyo ni jambo lisilo na shaka"

"Hilo nafahamu Stella"

"Sasa kwa nini unashituka? Kuna ajabu gani mtu kukualika kuhudhuria misa ya watakatifu wakati wewe ni Mkristo...?"

Isitoshe mtu aliyekutumia mwaliko huu pia amekutumia tiketi ya ndege, itakayokuwezesha kwenda Mwanza kesho jioni, ambayo ni siku moja kabla ya misa yenyewe, na kurudi Dar es Salaam siku inayofuata baada ya misa.

Itaendelea wiki ijayo...

Tangazo

NOTICE FOR CONVENING OF THE 26TH NATIONAL GENERAL CONVENTION

The Vice President of the Media Council of Tanzania (MCT) hereby notifies MCT members, in accordance with Article 13 of the MCT Constitution, that the 26th National General Convention (NGC) of the Media Council of Tanzania (MCT) will be held in Dar es Salaam on Friday, September 27, 2024. The Venue and time of the meeting will be determined in due course.

The proposed agenda at the 26th NGC is as follows:

1. Opening;
2. Adoption of Agenda;
3. Introduction & Remarks of newly appointed MCT Executive Secretary;
4. Confirming Minutes of the 25th National General Convention held at the African Court of People and Human Rights conference, in Arusha on September 28, 2023;
5. Matters arising from the 25th NGC;
6. Report of the Executive Secretary;
7. Adoption of 2023 Audited Financial Statements;
8. Appointment of External Auditor for the period ending December 31, 2024;
9. Election of MCT President/ Ratification of appointment of MCT President;
10. A.O.B;
11. Closing.

MCT members who have not paid their annual subscription fees by the deadline are reminded to do so immediately.

Yussuf Khamis Yussuf

Vice President
Media Council of Tanzania (MCT)

Complimentary Advert





Na Hellen NGOROMERA

Mapenzi hayataki mazoea katu



KARIBU msomaji wangu katika safu yetu ya mahusiano.

Leo tuendelee na mjadala kuhusu uhusiano katika ndoa. Tumeona kuwa mume na mke wote wana wajibu wa kuishi kwa upendo na furaha kuanzia wanapooana mpaka siku za mwisho wa maisha yao.

Hili ndilo litaimarisha ndoa yao. Mmoja akiamua kuacha kutekeleza jukumu hilo, ni dhahiri kuwa ndoa hiyo itayumba.

Na ndoa nyingi zinayumba hivi sasa kwa sababu wanandoa wengi wameacha kutekeleza jukumu hilo kikamilifu baada ya "kuzoeana" katika ndoa wakati kwa hakika mapenzi hayatambui huo uzoefu.

Katika familia nyingi, baada ya watu kufunga ndoa wanaona kama wameshamaliza na wanaacha kufanya mambo ya kukoleza pendo lao.

Mwanzo wa ndoa, wawili hao hufurahia maisha yao mapya kwa kuoneshana mahaba tele, wakiendeleza yale waliyokuwa wanayafanya wakati wakiwa wachumba.

Katika kipindi hicho cha awali, mke anajitahidi kumweka mumewe katika mazingira ya furaha zaidi kwa kumpatia huduma zote muhimu.

Lakini siku zinapokwenda na hasa baada ya kupata watoto, upendo baina yao huanza kupungua. Wengi wanadhani kuwa wazazi - hasa mama, anahamishia mapenzi kwa watoto badala ya mwenza wake.

Lakini hata bila kupata mtoto, baada ya kuishi na mume kwa muda mrefu kidogo, baadhi ya wanawake huacha kujijali, kujiweka nadhifu na hata kushindwa kuwahudumia waume zao ipasavyo.

Unaweza kukuta mwanamke ni mama wa nyumbani na mumewe ni mfanyakazi, lakini cha ajabu mumewe anaweza kurudi nyumbani na wala asimjali kwa chochote; asimfanye awe kivutio kwake, asimpatie huduma muhimu wala vitu vingine vizuri jambo ambalo linabomoa uhusiano wao.

Wanawake wengi wamekuwa wakiweka mazingira ya waume zao kuwa magumu, hivyo kuwa hatarishi kimapenzi!

Kuna wakati unaweza kumkuta mume wa mtu amevaa nguo chafu na zenye kutoa harufu, viatu vichafu, soksi mpaka mtu wa pembeni ukajiuliza kama ana mke!

Wapo wanawake ambao huwatuma wasichana wa kazi kufanya mambo muhimu ambao wao ndio wanapaswa kuyafanya kwa waume zao!

Wasichana wa kazi hutandika hadi vitanda wanavyolalia waliowaajiri, hufua nguo za ndani za baba wenye nyumba na mengine mengi ambayo yanapaswa kufanywa na mke.

Wiki iliyopita nilimsikia mchambuzi wa masuala ya ndoa na uhusiano, Vivian Pagazi, akisema wanawake wengi huaribu ndoa zao kwa kujitakia.

Nilimsikia akihoji mwanamke ambaye ni mama wa nyumbani anashindwaje kujitunza akamvutia mumewe?

"Wanawake wakishaingia kwenye ndoa hujitupa na kujiona wamemaliza kila kitu. Katika mazingira hayo hata mumewe akirudi nyumbani hawezi kumtamani kutokana na mazingira ya uchafu anayomkuta nayo..."

Mwanamke unatakiwa kumlea mumeo kwa mapenzi yote na kuepuka mazoea. Mume akirudi nyumbani mpokee kwa mahaba, mwandalie chakula ale ajisikie, siyo mumeo anarudi nyumbani anakukuta umekaa 'unachati' wala humjali.

Ni vyema sasa, ili kudumisha ndoa, wahusika waache mazoea, waone uhusiano wao ni mpya kila siku na hapo watadumu.

Tukutane wiki ijayo.

Kwa maoni na ushauri: hellen2ngoromera@gmail.com Au simu: 0754 88 67 49.

Mitindo & Urembo

Na Agatha Charles

Dondoo za kuvaa vyema kwa wanaume

WANAUME hawana mambo mengi katika mavazi, lakini katika hayo machache, bado kuna mahali baadhi wanakosea.

Wapo baadhi ambao hawajali kuhusu muonekano na wapo ambao kwao hilo ndio kipaumbele kwao.

Hapa naweka baadhi ya dondoo zitakasaidia mwanaume kuonekana nadhifu, anayevutia kwa kuwpangilia vyema mavazi yake.

Yakizingatiwa haya, hakika mwanaume atavutia kwa mavazi yake kila unapotoka nyumbani.

*Vaa kulingana na tukio

Hapa nazungumzia wanaume ambao wanaalikwa au kwenda sehemu yenye tukio fulani, mfano hafla ya chakula cha usiku, mkutano, harusi na nyingine.



Jitahidi uchague vazi linaloendana na sehemu na shughuli husika kwa wakati husika. Katika sehemu za mikutano vaa kiofisi ama suti.

Unapoamua kuvaa suruali ya jinzi kwenye sherehe ya harusi, jitahidi uvae shati usivae tisheti na usisahau kuongeza koti.

***Chagua kilicho bora na siyo wingi**

Mwanaume unaponunua nguo zako, angalia ubora na siyo wingi au bei nafuu. Ni bora uwe na shati moja la gharama kuliko kuwa na manne yasiyokuwa na ubora.

*Usione aibu kuiga

Siyo jambo la aibu kuiga iwapo mavazi unayoiga yatakuweka kwenye mwonekano mzuri.

Uelewe mwili wako na utendee haki.

*Vaa nguo zinazokutosha. Zisiwe kubwa kubwa wala ndogo sana za kubana.

*Usisahau kuwa kuna suti za kuvaa mchana na zile za kuvaa usiku.

Usije ukachanganya ya mchana ukavaa usiku, ya usiku ukavaa mchana.

*Uchaguzi wako wa shati jitahidi uwe wa hadhi yako. Juu panabeba mwonekano wa chini.

*Usisahau saa.

Hapa nazungumzia saa zinazotazamika. Yaani saa ambayo ukivaa mtu anaangalia mara mbilimbili.

*Mechisha mkanda na viatu.

Hapa ni muhimu kwani panakuongezea uwe na mwonekano wa kuvutia na kubeba upungufu wako kwenye mavazi ya siku husika.



Wanaume fanyeni scrub usoni

WANAUME wana desturi ya kutojali uso wao. Simaanishi wote, ila idadi kubwa hasa za wale wanaojiita wapambanaji huwa wanajisahau hata kupaka mafuta.

Leo nawakumbusha kuwa ngozi huwa zinachoka, hivyo zinahitaji kujaliwa kwa kufanya scrub angalau hata mara moja kwa wiki mbili haswa kwa uliyetingwa na mambo mengi.

Unapofanya scrub unaondoa ngozi iliyokufa na kuruhusu ngozi yenye nuru kujitokeza.

Scrub inarahisisha hata upumuaji wa ngozi pamoja na kukuweka sawa hata kama ulikuwa na uchovu.

Fanyia kazi suala hilo na utaona mabadiliko ya ngozi yako.

Kwa maoni na ushauri: piga simu 0656531217

Afcon



Suluhu Sports Academy iwe lulu Afcon

Na John MARWA

TANZANIA ni mwandaaji mwambata wa mashindano ya Mataifa ya Afrika mwaka 2027 - 'Pamoja Afcon 2027,' ambayo sasa iko kwenye maandalizi kuhakikisha mashindano hayo yanafanyika kwa ustadi na ubora wa hali ya juu.

Nchi zingine zinazoandaa kwa pamoja na Tanzania ni Kenya na Uganda.

Pamoja na kwamba nchi hizo zimeendelea na maandalizi ya Afcon 2027, ikiwemo ujenzi wa miundombinu ya viwanja, usafiri na usafirishaji, kuna maeneo mengi yenye mahitaji ya uwekezaji ambayo yakifanyiwa kazi, huenda Afcon 2027 ikawa ya mfano tangu kuanzishwa kwake.

Agosti 22, mwaka huu Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. Samia Suluhu Hassan aliweka jiwe la msingi la ujenzi wa Suluhu Sports Academy iliyoko eneo la Kizimkazi, Zanzibar. Huu ni wino ulikolezwa kwenye kitabu cha Afcon 2027.

Hii ni zaidi ya kuonyesha kwa vitendo kwamba matunda ya kuwa wenyeji yanaanza kuacha alama, hasa katika kuwaibua wachezaji nyota wa Afrika ambao wataingia kwenye vitabu vya kumbukumbu kwamba walifika Afrika Mashariki.

Rais ameonyesha ni namna gani taifa linapaswa kuwa na vituo vya kuibua na 'kuzalisha' vipaji ili kuweza kushindana kwa dhati katika mashindano mbalimbali.

Kuwa na 'Academy' zenye nguvu ya kiuchumi na uwekezaji wa kisasa ni dhahiri shahiri tutazalisha nyota wapya ambao soka la kisasa linawahitaji.

Mataifa yaliyoendelea kote duniani yana Academy zenye nguvu ambazo hutumika kuandaa mpango mkakati wa kuzalisha na kukuza vipaji adhimu.

Kule Ivory Coast, wenyeji waliopita wa Afcon 2023, kuna Academy ya Asec Mimosas, ambayo ni miongoni mwa vituo vilivyozalisha nyota wakubwa duniani kutoka Afrika ambapo – kwa muongo mmoja uliopita, majina kama Bonaventure Kalou na Didier Zokora yalianza kuchomoza.

Wengine ni Emmanuel Eboué, Bakari Koné, Gervinho, Salomon Kalou, Romaric, Boubacar Barry, Didier Ya Konan, Kolo Touré, Yaya Touré na Odilon Kossounou hao ni miongoni tu mwa wengi waliozalishwa pale Asec.

Kuwa na Academy yenye miundombinu bora, nguvu ya kiuchumi na falsafa nzuri ya kuwapata vijana wadogo, ndio silaha ya Asec Mimosas kufika walipo sasa.

Hapa ndipo yalipo maono ya Rais Samia na ujio wa Suluhu Sports Academy.

Ukiachilia nguvu ya kifedha inayoweza kuwekwa hapo, lakini ni kwa kiwango gani kituo hiki kitapata ushirikiano na vituo vingine vya kimataifa ili kuweza kubadilishana uzoefu na hata kuwapeleka kirahisi vijana wetu?

Ni wazi kuna mpango mahsusi kwa kituo hiki, Rais Samia anazidi kufungua pazia sekta ya michezo kwani ndio mkombozi wa ajira kwa karne hii.

Ni wakati sasa wawekezaji wengine kuamka na kuwekeza kwa nguvu kuungana na Rais Samia katika kuinua vipaji kwa vijana wetu, hasa kupitia michezo.





Diamond ‘avunja’ ndoa ya Zari

Johannesburg, AFRIKA KUSINI

UAMUZI wa Msanii Diamond Platnumz, kuhudhuria sherehe ya kuzaliwa kwa binti yao Tiffah, nchini hapa inaelezwa kuwa sababu ya kuvunjika kwa ndoa ya Zari the Boss Lady na mumewe, Shakib Lutaaya.

Kuvunjika kwa penzi la Zari na mumewe Shakib limefikia tamati, imejihidhilisha kupitia mitandao yao ya ‘Instagram’ ambapo kila mmoja amemuondoa mwenzake ‘unfollow’, huku wakifuta picha walizokuwa wamepiga pamoja.

Hivi karibuni, Diamond Platnumz, alihudhuria sherehe ya kuzaliwa ya binti yao Tiffah, huko Afrika Kusini kitendo ambacho kilipokelewa vibaya na Shakib na kuibua majibizano kwa wanandoa hao.

Hali hii ilisababisha kuwepo uvumi kuhusu hatma ya ndoa yao, iwapo inakaribia kuvunjika. Katika hali isiyoeleweka, wawili hawa walijibizana hadharani na kusambaza siri za ndoa yao kuwekwa hadharani.

Justin Bieber aongeza familia

New York City, MAREKANI

MSANII wa Pop kutoka Marekani, Justin Bieber na mkewe Hailey Bieber wamefanikiwa kupata mtoto wa kwanza wa kiume na wampa jina la ‘Jack Blues Bieber’.

Katika kuonyesha furaha yake Bieber ameposti kwenye mtandao wake wa kijamii, picha ya mguu wa mtoto huyo kwenye ukurasa wake wa Instagram na kisha kuweka neno la kumkaribisha nyumbani.

Msanii huyo katika kumkaribisha mtoto huyo ametumia wimbo wa ‘Burning’ wa msanii Tems kutoka Nigeria.

Nandy Festival, yaja kivingine

Dar es Salaam, TANZANIA

TAMASHA la Msanii wa Bongo fleva Faustina Charles Mfinanga maarufu kama ‘Nandy’ la ‘Nandy Festival’ linarejea kivingine.

Akitangaza kuhusu tamasha hilo, Nandy amesema linarejea ambapo kwa msimu huu ikiwa imebeba kauli mbiu ya ‘Tupishee’.

Msanii huyo ambaye ni mke wa rapa, Billnass akitangaza ujio huo akiwa ameongozana na mumewe.

Tamasha hilo huzunguka mikoa kadhaa nchini huku likisheheni nyota wa muziki wa bongo fleva, akisema tarehe rasmi atatangaza kupitia mitandao yake ya kijamii.



Williams

Winga Nico Williams kutoka klabu ya Athletic Bilbao ya Hispania, anatarajia kujiunga na washika mitutu wa London Arsenal kwa ada ya pauni milioni 75. Kama mambo yakienda vizuri huenda winga huyo akijiunga na Arsenal.

Ugarte



Klabu ya Manchester United yazidi kumnyemelea kiungo mkabaji wa Paris Saint-Germain (PSG), Manuel Ugarte kwa mkopo na chaguo la kumnunua msimu ujao, maongezi baina ya klabu hizo mbili yanaendelea vizuri.



Lukaku

Klabu ya Napoli imefikia makubaliano ya kumsajili mshambuliaji wa Chelsea, Romelu Lukaku aliyekuwa kwa mkopo msimu jana AS Roma, makubaliano binafsi baina ya mchezaji na klabu ya Napoli yamefikia pazuri.

Baada ya Kizimkazi, tujenge Kituo cha John Akhwari

Na Mwandishi WETU

WIKI iliyopita Rais Samia Suluhu Hassan aliweka jiwe la msingi la ujenzi wa Suluhu Sports Academy katika kijiji cha Kizimkazi, Kusini Unguja, Zanzibar.

Moja kati ya vitu vitakavyokuwemo kwenye academy hiyo ni uwanja mkubwa wa mpira wa miguu wenye uwezo wa kuingiza watazamaji 20,000. Huu ni uwanja mkubwa kuliko hata Uwanja wa Amaan, ambao ndio sura ya Zanzibar kwenye suala la michezo.

Inatambulika kuwa ujenzi wa uwanja huo utasaidia kupata viwanja zaidi kwa ajili ya fainali za Afcon mwaka 2027, ambazo Tanzania itakuwa mwenyeji pamoja na Kenya na Uganda.

Kuna miradi kadhaa ya ujenzi wa viwanja vya michezo ili kuhakikisha Tanzania inakuwa mwenyeji wa michezo hiyo kwa ufanisi.

Kwa ujumla, serikali imekuwa na juhudi kubwa kukuza michezo nchini, lakini juhudi hizo zinajidhihirisha zaidi kupitia mchezo wa mpira wa miguu kutokana na uwekezaji mkubwa unaofanywa kwenye eneo hilo ukilinganisha na michezo mingine.



Lakini ukiacha kucheza fainali za Afcon mara tatu, Tanzania haijawahi kupata mafanikio makubwa kwenye michezo kupitia mpira wa miguu.

Badala yake, mchezo wa riadha ndio ambao umeipa Tanzania sifa ya kidunia baada ya wanariadha wake kadhaa kufanya vizuri kwenye mashindano mbalimbali ya kimataifa.

Filbert Bayi na Suleiman Nyambui hadi leo wanaendelea kuweka alama kubwa, siyo hapa nchini tu, bali duniani kote kutokana na yale waliyoyafanya kwenye riadha.

Lakini pia yupo mwanariadha mwingine, John Akhwari, ambaye katika michezo ya Olimpiki ya 1968, licha ya kumaliza akiwa wa mwisho, aliacha gumzo kubwa duniani kote.

Alifika kwenye utepe ikiwa ni saa moja baada ya wanariadha wenzake wote kumaliza.

Aliingia katika uwanja wa michezo akipepesuka huku akitokwa damu akiwa na bendeji zilizokuwa katika mguu wake.

Akhwari alihojiwa na waandishi wa habari kwanini hakuacha mbio hizo baada ya kuumia, na jibu lake limebaki kuwa “mwanga” wa kuongeza hamasa, siyo katika michezo tu, bali maeneo mengi ya uwajibikaji.

Alijibu; “taifa langu halikunituma Mexico (ilikofanyika michezo hiyo) kuanza mbio, bali kumaliza. Ni uzalendo ndio ulionifanya kumaliza mbio hizo, licha ya kuwa nilikuwa na maumivu makali.”

Hivi tukiamua kuwekeza kwenye riadha na hata kujenga Akhwari Athletics Centre, kutakuwa na ubaya gani?



Mshambuliaji wa Simba, Steven Mukwala akishangilia moja ya bao alilofunga kwenye mchezo dhidi ya Fountain Gate FC jana. Kushoto ni Edwin Balua (Picha na Simba)

Simba, Yanga zang'ara, Azam, Coastal aaaah!

Na John MARWA

MNYAMA Simba hana kituo? Licha ya kuwa kikosi cha wekundu wa Msimbazi Simba kinajitafuta kupata ubora, muunganiko na makali ya kuwapepeta wapinzani bado hizo sio shida zao wameendelea kukanyaga tu mwendo na kuweka tatu kibindoni.

Vijana wa Kocha Fadlu Davis wamewachakaza Fountain Gate FC mabao 4-0 mchezo wa pili mzunguko wa kwanza wa Ligi Kuu Soka Tanzania Bara (NBC PL) 2024/25 katika Dimba la KMC Complex.

Kiwango bora kuanzia kwenye safu ya ulinzi chini ya Mousa Camara langoni, ubora wa safu ya kiungo mabegani mwa Fernandes Mavambo huku utuli wa kufumania nyavu ukithibitishwa na MVP Jean Charles Ahoua mnyama katakata haswa.

Mabao ya Edwin Balua, Steven Mukwala, Jean Chalres Ahoua na Valentino Mashaka yalitosha kuwakaribisha Fountain Gate kwenye ulingo wa NBC PL. Kwa matokeo hayo Mnyama anakaa kileleni mwa msimamo na pointi 6 mabao 7 huku hawaruhusu bao.

Jean Charles Ahoua amezidi kudhihirisha ubora wake taratibu kwa kuonyesha kiwango bora akihusika kwenye mabao 4 kati ya saba ambayo Simba wameyaweka kambani, akifunga bao 1 na pasi za usaidizi wa mabao 3.

Wakati Mnayama akizidi kufanya yake watani zake Yanga SC nao katika mashindano ya Ligi ya Mabingwa walikamilisha kibarua cha kuwaondosha Vital'O ya Burundi kwa jumla ya mabao 10-0 baada ya August 24 kuwasasambua mabao 6-0 mchezo wa pili wa hatua za awali.

Kwa upande wa Azam FC wao Bundi amezidi kutanda katika mitaa yao na maisha ya michuano ya kimataifa kwa kuondoshwa na APR ya Rwanda kwa jumla ya mabao 2-1, baada ya APR kuibuka na ushindi wa 2-0 mchezo wa pili ulipigwa jumamosi iliyopita katika Uwanja wa Amahoro Kigali nchini humo.

Nao Wagosi wa Kaya wameumaliza mwendo kwa kuondoshwa kwenye hatua za awali na Bravos ya Angalo katika Kombe la Shirikisho kwa jumla ya mabao 3-0 baada ya kukubali kisango cha mabao hayo kwenye mchezo wa mkondo wa kwanza ulipigwa nchini Angola na kusuluhu Azam Complex.

Rasmi Tanzania imesaliwa na timu mbili kati ya nne kwenye mashindano ya klabu ya Shirikisho la Soka Afrika CAF, ambapo Yanga anaingia hatua ya kwanza CAF CL na Simba hatua ya kwanza ya CAF CC.

GAZETI hili lilianzishwa 2021, kuandaliwa na kusambazwa na Chama cha Waandishi wa Habari Tanzania (Tampa) na kusajiliwa na Serikali ya Tanzania, kupitia Idara ya Habari (MAELEZO) na kupewa leseni namba - 00000448. Linaendeshwa kwa ushirikiano wa mzunguko – kwa kila nchi, wa mwaka mmoja na waandishi wa Tanzania, Kenya, Uganda, DRC na Rwanda.

TAMPA
TANZANIA MEDIA PRACTITIONERS ASSOCIATION